SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 260,838,830
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




UKURASA 4

**WAMILIKI** maduka dawa muhimu walalamika kuhamishiwa nje ya mji


Nipashe Spotika

SABABU 3 KWA NINI NUNEZ ATAFANIKIWA LIVERPOOL

UKURASA 11

Jumatatu Juni 20, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580982

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Aibu mkoa wangu kuwa wa mwisho ufaulu

UKURASA 2




Rais Samia Suluhu Hassan (katikati), akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi rasmi wa Taasisi ya Mwanamke Initiative (MIF) Zanzibar jana, hafla hiyo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa Bara na Visiwani. Wengine ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wapili kushoto), Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamad Mussa (kushoto), Mwenyekiti na Mwanzilishi wa Taasisi ya Mwanamke Initiative (MIF), Wanu Hafidh Ameir, pamoja na Ofisa Mtendaji Mkuu wa taasisi hiyo, Fatma Mwassa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 3

## AHUKUMIWA KUNYONGWA HADI KUFA KWA MAUAJI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza imemhukumu, Damiani Andrea (62), kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumpiga risasi na kumuua...

UKURASA WA 5

## WAKUU SEKONDARI ZA SERIKALI WAONYWA MICHANGO

WAKATI serikali ikitangaza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita nchini, Mkuu Mkoa wa Dodoma...

UKURASA WA 9

## NIPASHE YASAIDIA MTOTO MWENYE KICHWA KIKUBWA

SHIRIKA la Child Help Tanzania (CHT) limesema litasaidia matibabu ya mtoto Collin Msambwa, mwenye umri wa miezi mitano...

# Wanafunzi 4 walivyofariki kwenye bodaboda inayodaiwa kuazimwa

UKURASA 2

## CHADEMA yageukia wabunge kupanda gharama za maisha

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YAONYESHA UKUBWA WAKE CAF UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Dk. Caroline Nombo (kushoto), akikagua moja ya vifaa vya mafunzo ya wahandisi wa matengenezo ya ndege baada ya kuvizindua katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) jijini Dar es Salaam mwishoni nwa wiki. Wengine ni Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Zacharia Mganilwa (watatu kulia) na Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi wa chuo hicho, Prof. Blasius Nyichomba (Wapili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia: Aibu mkoa wangu kuwa wa mwisho ufaulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema hafurahishwi na matokeo ya mitihani ya taifa ya kidato cha nne na sita ya Shule za Zanzibar hasa Mkoa wa Kusini Unguja kwa kushika nafasi za mwisho.

Alisema ni aibu mkoa anaotoka Rais (Mkoa wa Kusini Unguja) kufanya vibaya katika mitihani ya taifa ikilinganishwa na mikoa mengine.

Aliyasema hayo jana wakati akizindua Taasisi ya Mwanamke Initiatives (MIF), visiwani hapo.

Aipongeza juhuzi za MIF na Serikali ya Zanzibar kwa kupania kuhakikisha wanapunguza tatizo la ufaulu mdogo visiwani humo.

"Kawaida mitihani inapomalizika, Wizara ya Elimu Tanzania hunimletea mavitabu makubwa ya matokeo ya mitihani na flashi au CD ya kuonesha mitihani yote, na ninapoweka flash katika kompyuta yangu kwanza nakwenda katika Mkoa wa Kusini Unguja na ninapoona matokeo nashika kichwa... Mungu wangu ehee, nini hiki sasa, ni aibu, Rais wa Tanzania mkoa aliotoka upo mwisho," alionyesha kusikitika Rais Samia.

Hata hivyo, alisema amevutiwa na maelezo ya Serikali ya Zanzibar kuhusu mabadiliko makubwa kukabiliana na changamoto hiyo ya ufaulu.

Aliyataja mabadiliko hayo kuwa ni uboreshaji wa mitaala ya kufundishia ili kutoa elimu yenye tija, kuweka kipaumbele kwenye mafunzo ya amali na kudhamiria kujenga shule 10 za mafunzo hayo, kuongeza shule za ufundi kila wilaya, na kuongeza ajira za walimu zaidi ya 4,000 kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema ni hatua kubwa na zinaleta matumaini ya kupunguza tatizo la ufaulu mdogo.

Aliitaka serikali kuajiri walimu wenye sifa, wa kujitolea ambao wameshaonyesha uwezo wao, pia kuwapima walioajiriwa na kuangalia wanaofanya vizuri na wasiofanya vizuri, waweze kujituma na kufundisha vizuri wanafunzi.

Aidha, alisema ili Zanzibar iwe na matokeo mazuri ya wanafunzi katika mitihani yao ya taifa ni lazima kuwapo ushirikiano kati ya wazazi, walimu na serikali huku akiwataka wazazi hao kufuatilia maendeleo ya elimu ya watoto wao.

"Changamoto ya elimu Zanzibar ni jukumu letu sote hatuna wa kumtupia lawama na ili wanafunzi wafaulu vizuri, jitihada za walimu, wazazi, sekta binafsi na serikali na wanafunzi wenyewe zinahitajika," alisema.

Rais Samia alisema sio suluhisho mtoto anaposhindwa kufaulu kupewa mume, ni vyema kuwasomesha watoto wa kike na wakiume ili kwa pamoja wasonge mbele kimaendeleo.

Aliitaka jamii kushirikiana kuwalea watoto vizuri kwa sababu wasipowalea vizuri watazalisha watoto watukutu wanaojiingiza kwenye makundi yanayofanya vitendo viovu kwenye jamii.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, alisema serikali itaendelea kuiunga mkono taasisi hiyo ambayo imekusudia kuboresha sekta ya elimu Tanzania.

Alisema maono ya taasisi hiyo yanafanana na ya serikali katika kutekeleza suala zima la utunzaji wa elimu Zanzibar na serikali ina mpango wa kujenga vyuo vya ufundi katika wilaya zote visiwani humo ili kuwasaidia vijana kupata fursa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa, aliipongeza taasisi hiyo kwa jitihada zao za kuwakomboa vijana kitaaluma lengo likiwa kuleta maendeleo ya kijamii na taifa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa MIF, Wanu Hafidh Ameri, alisema changamoto za kijamii ni nyingi na zinahitaji nguvu za pamoja kuzitatua kwa kuamua kuunga mkono juhudi za serikali kusaidia kutatua changamoto hizo.

Alisema wameelekeza nguvu kubwa katika elimu, kwa kuwa ndiyo nyenzo muhimu itakayomsadia kijana husasan msichana kuendesha maisha yake na kuepuka udhalilishaji.

"Tunalenga kubadili maisha ya vijana waondokane na umaskini, tukielekeza nguvu kubwa za kuinua kiwango cha ufaulu na wale wenye utashi wapatiwe mafunzo ya ufundi nawaomba wadau wote watuunge mkono," alisema Wanu.

# Wanafunzi wanne walivyofariki kwenye bodaboda inayodaiwa kuazimwa

**Na Beatrice Shayo**

WANAFUNZI wanne wamefariki dunia papo hapo eneo la Mapinga, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, baada ya pikipiki iliyokuwa ikiendeshwa na mmoja wao inayodaiwa kuazimwa, kugongwa na lori.

Wanafunzi waliofariki wametajwa kuwa ni Arnold Boniface na Samrati Masoud, wanasoma kidato cha tatu Shule ya Sekondari Mapinga.

Wengine ni Rahma Kitindi anayesoma kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Mapinga, pamoja na Idrisa Masoud anayesoma darasa la nne Shule ya Msingi Mtambani.

Akizungumza na Nipashe kuhusu ajali hiyo, Diwani wa Kata ya Mapinga, Chandika Dismas, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa moja usiku katika eneo hilo.

Akisimulia tukio lilivyotokea, alisema wanafunzi wote walikuwa wamepanda kwenye bodaboda hiyo na mmoja wao (Arnold Boniface) ndiye aliyekuwa akiwaendesha wenzake.

Diwani huyo alisema, wakati wanaingia barabarani mwanafunzi mwenzake alimshtua dereva wao kuwa kuna lori linakuja, na aliposhtuka ghafla aligonga kingo ya barabara na kuangukia barabarani hali iliyosababisha kukanyangwa na lori hilo.

"Wanafunzi hao walivyoangukia barabarani lori lilikuwa katika mwendo kasi na kuwakanyaga wote wakiwa wamelala barabarani," alisema Dismas.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, aliwatafuta wenyeviti wa vitongoji na kuwapa taarifa kuhusu ajali hiyo.

Dismas alisema alikwenda Kituo cha Afya Kerege na kuomba kuingia katika chumba cha kuhifadhia maiti ili kuwatambua wanafunzi hao japo alishindwa kutokana na hali zao na kushindwa kuwatambua.

"Huyu mwanafunzi Arnold Boniface aliweza kutambulika kwa sababu hiyo pikipiki aliazima, na dereva akamtaja na kujulishwa wazazi wake," alisema Dismas. "Nilirudi kwenye familia ya Boniface huku nikiwa najiuliza wale watoto watatu ni wa kina nani, nikataka kila kitongoji waeleze kama kuna nyumba ambayo mtoto hakurudi nyumbani."

Dismas alisema Mwenyekiti wa Kitongoji cha Kwa Kibosha alimjulisha taarifa ya msiba na kumtajia majina ya wanafunzi hao waliofariki katika ajali hiyo.

Alisema wazazi baada ya kutambua miili ya watoto wao iliwalazimu kuwazika kutokana na hali zao kuwa mbaya.

"Mpaka sasa tumeshawazika watoto watatu, mwanzo ilikuwa wawili wanasafirishwa, lakini tulipokuwa tunazika huyu mwingine tukaambiwa wanachimba kaburi kumzika mtu wa tatu kwa sababu hali yake ni mbaya hawataweza kumsafirisha," alisema Dismas.

Alisema Anord Bonifance wamepanga kumsafirisha kwa ajili ya mazishi mkoani Mbeya.

"Tatizo lililojitokeza ni hawa madereva wakiwaona wanafunzi wana umri wa miaka 18 wanawapa bodaboda kinyume cha sheria," alisema Dismas.

Alisema katika eneo hilo ni muda mrefu wameiandikia barua Wakala wa Barabara (TANROADS) wakiwaomba waweke matuta kwa sababu malori yanapita kwa mwendo kasi lakini mpaka sasa imeshindikana.

Dismas alisema: "Hata mbunge wetu ameliongelea hili sana. Tumeandika barua TANROADS kuomba matuta mpaka sasa hakuna, hili eneo ajali zinajitokeza mara kwa mara na malori yanapita kwa spidi kwa sababu hakuna alama."

Nipashe lilimtafuta Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Gregory Mushi, ambaye alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, akizungumza na wananchi wa Wilaya ya Manyoni katika mkutano wa hadhara uliofanyika juzi mjini Manyoni kwa lengo la kusikiliza kero zao. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# CHADEMA yageukia wabunge kupanda gharama za maisha

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema mijadala inayoendelea bungeni haigusi mambo muhimu ya kufanyiwa marekebisho katika bajeti ya serikali iliyowasilishwa.

Chama hicho kimebainisha mambo yanayotakiwa kujadiliwa kuwa ni kupanda kwa gharama za maisha na mchakato wa katiba mpya.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Manyika, akizungumza jijini Dar es Salaam jana kuhusu tathmini ya bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23, alisema mpaka sasa inaonyesha Bunge halitekelezi ipasavyo wajibu wake wa kuishauri serikali kuhusu hotuba zake zinazowasilishwa bungeni.

Akifafanua kuhusu tathmini hiyo, alisema michango inayotolewa na wabunge katika mhimili huo wa kutunga sheria haichambui masuala muhimu ya udhaifu na upungufu ulioko katika hutuba zilizosomwa bungeni.

Alishauri kwa siku chache zilizobaki za kuhitimisha vikao vya Bunge mjadala wa bajeti na sheria ya fedha vifanyiwe marekebisho ya msingi hususani upungufu uliopo kwenye bajeti iliyowasilishwa.

"Iwapo rai zitakazotolewa zisipofanyiwa kazi na Bunge likapitisha bajeti bila kuzingatia masuala ya msingi, isiwe kikomo cha kuendelea na uchambuzi, kuwawakilisha na kusema kwa niaba ya wananchi, mpaka mabadiliko ya msingi yafanyike kwa manufaa ya Watanzania.

"Tumefanya tathmini ya kina ya bajeti, hotuba ya waziri na uchambuzi wa vitabu vya bajeti za wizara mbalimbali, katika uchambuzi wetu tumebaini kwamba suala ambalo ni rai ya wananchi ya muda mrefu ya kurejeshwa na kukamilishwa kwa mchakato wa katiba mpya halijatengewa fedha za kukamilishwa kwake".

Mnyika alizungumzia mpango wa taifa wa maendeleo juu ya utawala bora, uimarishaji wa demokrasia na mifumo ya kiutawala kama msingi mmojawapo katika hatua za maendeleo ya nchi.

Alisema kwa muktadha huo, mchakato wa kukamilisha katiba mpya uingizwe kwenye bajeti ya serikali kama moja ya miradi ya kipaumbele.

"Hii bajeti sio ya wananchi na sio ya wote kwa sababu haizingatii matakwa ya wote ikiwamo ya wananchi wanaotaka kuwa na katiba mpya," alisema Mnyika.

Alitoa wito kwa Bunge na wananchi kuendelea kupaza sauti kuhusu ongezeko la bei ya mafuta, kuitaka serikali kupunguza tozo na kodi ambazo zinachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la bei ya bidhaa hiyo ili kuwanusuru wananchi na mzigo wa kupanda kwa gharama za maisha.

Alisema wakati umefika kwa serikali kutekeleza mapendekezo iliyoyatoa ya kupunguza gharama za uendeshaji na matumizi mengine yasiyo na ulazima ili kuelekeza fedha katika masuala ya msingi ya maendeleo.

Alishauri serikali kuongeza nguvu zaidi katika utekelezaji wa kisera na bajeti, akidai kuwa hatua walizoziona hadi sasa hazijitoshelezi kuwezesha nchi kujitegemea kwenye bidhaa ambazo wana uwezo wa kuzizalisha nchini.

"Tunaona bajeti ya serikali haijaweza kuchukua hatua za kutosha za kuiwezesha sekta binafsi kuwa kipaumbele kwenye uwekezaji, kilimo na sekta nyingine ambazo zinaweza kuchangia katika kupunguza gharama za maisha kwa wananchi, tunataka hatua za serikali kwenye eneo hili.

"Tumeona pia hotuba ya bajeti ya serikali haijagusa kwa ukamilifu wake hatua za haraka za uwekaji wa miundombinu ya utumiaji wa gesi kwenye magari na viwandani ili kupunguza gharama, pia hatujaona hatua katika utumiaji wa nishati mbadala mikoa inayozalisha umeme kwa kutumia mafuta, tunatoa wito jambo hili lipate kipaumbele."

Kwa upande wa Bunge na wadau mbalimbali, kuitaka serikali ieleze hatua ambazo imechukua katika kushughulikia masuala yote ya ufisadi, rushwa na matumizi mabaya ya fedha za umma yaliyoelezwa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kadhalika, alitoa wito kwa serikali kuwa na mpango maalumu wa kushughulikia kupanda kwa gharama za maisha na kuingiza vifungu kwenye muswada wa sheria ya fedha ili ifikapo Julai mosi, bei ya mafuta ishuke kwa kiwango ambacho kitaleta unafuu kwa wananchi.

# Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza imemhukumu, Damiani Andrea (62), kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kumpiga risasi na kumuua mfanyabiashara wa madini, Samwel Songoma.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa mahakama hiyo, Lilian Itemba, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha kosa hilo pasipo shaka. Jaji Itemba alisema mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na watu wengine wenye tabia ya kikatili. Aidha Jaji Itemba alisema upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Janeth Kisibo, alipeleka mahakamani mashahidi tisa na vielelezo 10 ambavyo vilithibitisha kuwa mshtakiwa huyo alimuua Songoma kwa kumpiga risasi tumboni na kufariki.

Jaji Itemba alisema shahidi wa nne ambaye ni mke wa marehemu siku ya tukio alikuwa amelala na mume wake usiku majambazi walifika na kuvunja mlango na kuingia ndani na kuamuru mumewe (Samweli Songoma) kutoa fedha.

Alisema Songoma alitoa fedha ambazo shahidi huyo hakujua ni kiasi gani, baada ya majambazi hao kupewa fedha walizunguka nyuma ya nyumba na kubomoa dirisha likaanguka juu ya kitanda.

Alisema Songoma aliendа kujificha kwenye kona ya nyumba na shahidi ambaye ni mke wake alijificha chini ya kitanda.

Alisema majambazi hao walimulika tochi na kumuoma Songoma akiwa amejificha kwenye kona ya nyumba hiyo kwa ndani.

Jaji Itemba alisema majambazi baada ya kumuona Samweli kwenye kona walimlazimisha kuongeza fedha zingine, hata hivyo aliwajibu kuwa hana.

Baada ya kupewa jibu hilo, majambazi hao walimpiga risasi ya tumboni na kufariki hapo hapo.

Aidha, Jaji Itemba alisema majambazi watatu waliingia ndani na kuanza kupekua vitu ndani ya chumba hicho wakitafuta fedha. Alisema wakati wakiendelea kupekua mke wa marehemu alimtambua jambazi mmoja kwa jina la Damiani Andrea kwa sababu alikuwa amekatika mkono wa kushoto, pia alikuwa ni fundi ujenzi katika Kijiji cha Lyobaika, Wilaya ya Bukombe.

Alisema baada ya majambazi hao kumaliza kupekua waliondoka na kutokomea kusikojulikana ndipo mke wa marehemu alipata nafasi ya kupiga kelele kuomba msaada wa majirani.

Jaji alisema marehemu alipelekwa Hospitali ya Geita na daktari aliyefanya uchunguzi wa mwili alidai kuwa kifo cha marehemu kilitokana na damu kuvilia ndani ya tumbo kutokana na kupigwa risasi chini ya kitovu na kupasua mishipa ya damu. Alisema Songoma alikuwa akifanya biashara ya kuuza dhahabu katika Kijiji cha Lyobaika Wilaya ya Bukombe mkoa wa Geita.

Baada ya kutoa adhabu hiyo, Jaji Itemba aliagiza bunduki moja, risasi 72 na magazine tatu vyote kwa pamoja vitaifishwe na vipelekwe serikalini baada ya muda wa rufaa kumalizika.


**KUPOTEA KWA CHETI**



**DEOGRATIAS R. PAUL**

Anatangaza kupotelewa kwa cheti cha kidato cha nne mwaka 1985 namba ya cheti **S.118/5**. Yeyote atakaе kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**URP/RB/7988/2016**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**Tarehe: 20/06/2022**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote na wafanyabiashara kwamba kutakuwa na mnada wa hadhara wa uuzaji wa miti katika viunga/vitalu vya shamba la Halmashauri eneo la Nkunga katika Kijiji cha Ibililo. Mnada huu utafanyika tarehe 28/06/2022 siku ya Jumanne saa 5:00 asubuhi katika eneo la msitu.

**Vitalu vitakavyouzwa kwa mnada pamoja na vipimo vyake ni kama ifuatavyo:-**

| Plot No. | Idadi ya miti | Ujazo ($M^3$) kwa miti yote | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | 49 | 27.777 | |
| 2 | 48 | 19.547 | |
| 3 | 28 | 8.419 | |
| 4 | 110 | 25.049 | |
| 5 | 126 | 41.146 | |
| 6 | 148 | 36.257 | |
| 7 | 97 | 30.479 | |
| **Jumla** | **606** | **188.674** | |

2. Kiunga kitanadiwa kulingana na idadi ya miti iliyopo. Mnada huu utakuwa kwa jamii yote, hivyo Kampuni au Mtu binafsi mwenye nia ya dhati ya kununua miti ataruhusiwa kushiriki.

3. Watu binafsi na Makampuni wanakaribishwa kutembelea eneo la shamba la miti kwa gharama zao wenyewe siku mbili kabla ya tarehe ya mnada kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri, Afisa Misitu husika atakuwepo shambani hapo kwa ajili ya maelekezo zaidi.

**Masharti ya Mnada**

i. Mnunuzi atakayetaja bei ya juu ndiye atakayepata zabuni husika. Na kwamba atatakiwa kulipa fedha 45% ya bei ya thamani ya miti iliyonunuliwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kitatakiwa kulipwa ndani ya siku saba (7) tangu siku ya mnada na kwamba kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa kwa mnunuzi na mnada utarudiwa tena.
ii. Mnunuzi atatakiwa kuvuna miti na kuiondoa katika eneo la shamba ndani ya muda wa siku thelathini (30) kuanzia siku ya kukamilisha malipo ya mwisho ya asilimia Hamsini na Tano (55%).
iii. Ruhusa ya kuangalia eneo la shamba la miti itatolewa siku mbili (2) kabla ya tarehe ya mnada.
iv. Mnunuzi aoneshe nia thabiti ya ununuzi vinginevyo kuvuruga mnada pasipo na nia thabiti ya ununuzi, sheria itachukua mkondo wake.
v. Mnunuzi atapaswa kufuata taratibu zote za kufanya biashara ya mazao ya misitu (kwa mujibu wa Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 na Sheria ndogo ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe).
vi. Mnada utaanza saa 5:00 asubuhi tarehe 28/06/2022 siku ya Jumanne eneo la shamba la Nkunga katika Kijiji cha Ibililo.

4. Imetolewa na,

**Mchau, R.B**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

216908901



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani na wafanyakazi wa kampuni ya usambazaji magurudumu ya Superdoll, wakikagua mabasi, kabla hayajaanza safari za kwenda mikoani, kwenye stendi ya Magufuli, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wamiliki maduka dawa muhimu walalamika kuhamishiwa nje ya mji

**Na Jenifer Gilla**

WAMILIKI wa maduka ya dawa muhimu za binadamu wamelalamikia kitendo cha Baraza la Famasi kuwanyima vibali vya biashara na kufungia maduka yao kwa amri ya kuhamia vijijini, kinaua biashara zao na kurudisha nyuma maendeleo yao.

Walitoa malalamiko yao walipokuwa wakiongea na Nipashe na kuiomba serikali kuangalia upya uamuzi huo ambao pia unasababisha maisha yao kuwa ya kuhama mara kwa mara mji unapotanuka.

Mmoja wa wamiliki wa maduka hayo, Josephine Bura (46), alisema alifungua duka lake mwaka 2006 eneo la Kibangu Msikitini, biashara iliyomsaidia kujenga nyumba maeneo hayo na kwamba amri ya kuhama anaiona ikimrudisha nyuma.

"Fikiria nimepambana kujenga kibanda changu hapa ili kupunguza ukali wa maisha, ninavyoambiwa nihamie kijijini ninakwenda kuishije na familia hii, nitamudu vipi kulipa kodi ya nyumba, kibanda cha biashara na kusomesha watoto watatu kwa kutegemea biashara hii moja," alilalama Josephine.

Josephine ambaye analea watoto wake mwenyewe, alisema kwa sasa maisha yake yamerudi nyuma kutokana na kutofungua biashara hiyo mara kwa mara kuhofia kufungiwa kama amri inavyowataka.

"Zamani nilikuwa kwa siku nauza Sh. 50,000 hadi laki, faida hapo naweza kupata 20,000 hadi 50,000 kwa siku, lakini kwa sasa naweza kukaa wiki nzima nikapata Sh. 5000, sielewi hawa watoto wasio na baba niwapeleke wapi," alilalamika Josephine.

**KUHAMAHAMA**

Joyce John (42), alilalamikia kitendo cha kuhamishwa kunasababisha kipato chake kushuka na kuwa mtu wa kuomba misaada kwa ndugu.

Akiwa na familia ya watoto wawili, anasema alifungua duka hilo eneo la Changanyikeni mwaka 2010 baada ya kusimamishwa kazi na kuamua kwenda kupata mafunzo ya uuzaji wa dawa ili kuwa na kigezo cha kupata kibali.

"Baada ya kupata mafunzo mwaka 2013 nikafuatilia kibali, nikaambiwa jengo langu dogo halikidhi viwango nikaongea na mwenye nyumba nikaongeza jengo kwa gharama zangu, kisha nikamwita ofisa afya akakagua akasema sasa ninaweza kufuatilia kibali, nilipokwenda kuomba kibali nikaambiwa eneo hilo ni mjini yanatakiwa maduka makubwa ya dawa hivyo nihamie nje ya mji, kwa kweli nilichanganyikiwa," alisema Joyce.

Kwa mujibu wa mama huyo baada ya kufuatilia kibali bila mafanikio na kuishi maisha ya kufanya biashara kwa kujificha kwa muda mrefu toka mwaka jana (2021) akafanya uamuzi wa kuhamishia biashara yake nje ya mji.

Alisema alipata eneo la Msewe, Manispaa ya Ubungo ambalo liliorodheshwa kama moja ya maeneo yanayoruhusiwa kuhamia na alipofuatilia kibali akaambiwa kuwa kumeshakuwa mjini, aende eneo la Golani.

Abdulrahman Haji (56), anayemiliki duka la dawa Tandale, alisema kuondolewa kwenye eneo lake la biashara alilowekeza tangu mwaka 1997 kumemwathiri kwa kuwa hana uwezo wa kufungua pharmacy.

"Huu ni uonevu dadangu, utanikatazaje kufanya biashara kwenye eneo langu kisha uniambie niende nje ya mji nikapange hizo gharama nitazimudu vipi na nina familia inanitegemea. Gharama za kuendesha pharmacy ni kubwa mimi sina uwezo huo," alilalamika Abdulrahman.

**KIINI CHA TATIZO**

Mwenyekiti Taifa wa CHAMA cha Wamiliki wa Maduka ya Dawa Muhimu za binadamu (UWADAMUDA), Juma Mganga, alisema waliambiwa wahamie nje ya mji mwaka 2010 baada ya kuwa wametimiza vigezo vyote vinavyohitajika kumiliki maduka hayo.

"Kwanza walituambia twende tukapate mafunzo ili tuweze kusimamia maduka hayo, tukatoa pesa zetu Sh. 300,000 kila mmoja, tukasoma mafunzo ya ADO mwaka 2012 baada ya hapo tukapewa taarifa kuwa kuna sheria imetungwa tuhame mijini kwenda vijijini," alisema.

Mganga ambaye ni Mwenyekiti wa wamiliki wa Maduka ya Dawa Muhimu Mkoa wa Dar es Salaam, alisema ombi lao kwa serikali ni kuwawezesha kupewa vibali vya kuendelea kufanya shughuli hiyo mjini.

**MGONGANO KIMASLAHI**

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Mwadini, alisema anaona kuna mgongano wa kimaslahi kwa kuwa mamlaka zinazosimamia tasnia ya maduka ya dawa wengi wao ni wamiliki wa maduka makubwa ya dawa.

"Inakuwaje Baraza la Pharmacy litusimamie sisi wakati na wenyewe ndiyo wanaomiliki maduka, wanasimamiwa na nani? Tunataka mamlaka zilizo juu na zenyewe zione hili wajue wapo mungu watu wametokea kwenye tasnia hii," alisema.

Kwa mujibu wa Abdul, moja ya vigezo vinavyotakiwa katika kumiliki famasi ni kuajiri mtu aliyehitimu ufamasia ambaye anatoka kwenye baraza hilo na kudai kuwa gharama za kumlipa ni kubwa.

"Kumlipa mfamasia si chini ya Shilingi milioni moja kwa mwezi, halafu sio kwamba ndiyo atakaa dukani auze, hapana anakupa tu cheti chake kama ushahidi, lakini yeye hakai hapo, mfamasia mmoja anaweza kutumika na maduka matatu, kwa hiyo mimi naona hawa wenzetu wanataka kujitengenezea mazingira ya kujinufaisha wao," alilalamika.

Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Mwadini, alisema kuwa kutokana na kunyimwa kibali hicho baadhi ya wamiliki wa maduka wamelazimika kufanya biashara bila kulipa kodi ya mapato (TRA) na manispaa kwa sababu wakienda kufuatilia leseni na TIN wanaambiwa waambatanishe vibali kutoka baraza lao.

"Baada ya kushinda kesi mahakamani tukawa tunafanya biashara kwa amri ya mahakama, lakini hatuna uwezo wa kulipa mapato ya serikali kwa sababu hatuna kibali cha kuambatanisha," alisema.

Ofisa Biashara wa Manispaa ya Ubungo, Prisca Mjema, alisema kuwa baada ya kuona wamiliki hao wanaendelea na biashara bila kulipa kodi huku serikali ikikosa mapato, wakaamua kuwapa njia ya kulipia mapato hayo.

"Tukawa tunawatembelea katika maduka yao tunawapa namba ya kulipia kodi kisha tunawapa risiti ili wakishapata vibali tutakuja kuwapa leseni zao," alisema Prisca.

**MSAJILI ANENA**

Alipotafutwa kuzungumzia sakata hilo. Msajili wa Baraza la Famasi, Elizabeth Shekalaghe, alisema hana cha kuzungumza zaidi ya kuwataka wamiliki hao kufuata sheria na taratibu za usajili.

"Ukisoma sheria au kanuni inasema kwamba yale maduka yanatakiwa yawe maeneo fulani, ndivyo sheria inavyosema sasa ni issue gani mimi sina majibu hayo," alijibu kwa kifupi.

# Naibu Waziri akagua uoteshaji, upandaji miti

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, ametembelea na kukagua upandaji miti katika maeneo mbalimbali jijini Dodoma.

Upandaji wa miti hiyo ulifanyika katika barabara ya Ihumwa – Iyumbu, Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Medeli, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Iyumbu, kwamba Naibu Waziri huyo aliridhishwa na usimamizi, ufuatiliaji wa miti hiyo tangu ilipopandwa.

Hivyo, alitoa pongezi kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Jiji la Dodoma, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na wadau mbalimbali wanaotoa mchango katika utunzaji wa miti.

"Leo tumefanya ziara ya kukagua miti ambayo imepandwa kwa sababu kuu mbili moja ni sera yetu ya mazingira inatuelekeza tupande miti na kuiendeleza ili tujue ipi imeota na ipi imekufa, lakini tunafanya ziara hii kufuatia maelekezo ya Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, ambaye kwa nyakati mbalimbali amekuwa akitusisitiza kufuatilia miti inayopandwa," alisema.

Aidha, Naibu Waziri Khamis alitoa wito kwa wadau mbalimbali wa mazingira kuwa na ushirikiano katika kuhakikisha miti inaoteshwa na kutunza ili kutimiza azma ya kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa na hivyo kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

Aliwasihi TANROADS wawe wanawafuatilia watu waliowapa zabuni ya kumwagilia miti kuwa wafuatilie zoezi hilo kama linafanyika kwa mujibu wa utaratibu uliopangwa.

Meneja Msaidizi wa Maendeleo ya Rasilimali Misitu kutoka TFS, Patricia Manonga, alisema Programu ya Dodoma ya Kijani wanatarajia kuongeza uzalishaji wa miche kutoka milioni moja hadi milioni mbili kwa mwaka kupitia kitalu kilichopo Mailimbili.

Alisema hadi kufikia sasa tayari TFS imezalisha miche zaidi ya milioni 57 ambayo imepandwa katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma, kwamba zoezi rasmi lilizinduliwa mwaka 2017.

Akitoa mchanganuo wa miti iliyopandwa, Patricia alifafanua kuwa katika eneo la Medeli ilipandwa miti 500, Iseni miti 1,200 na Iyumbu ilipandwa miti ya kivuli takriban 1,000, hivyo alizitaka taasisi kupanda miche wanayopatiwa badala ya kuiacha ikaharibika.

# Wakuu sekondari za serikali waonywa michango

**Paul Mabeja na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKATI serikali ikitangaza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita nchini, Mkuu Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewaagiza wakuu wa shule za sekondari za serikali kufuta michango yote isiyokuwa na tija ili kuwezesha wote walichaguliwa kujiunga na shule bila kusumbuliwa.

Aidha, amesema michango itakayotakiwa kuendelea kutolewa ni inayohusu mambo ya msingi na muhimu kwa wanafunzi na sio vinginevyo na isizidi Sh. 150,000 kwa kila mwanafunzi.

Alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na wakuu wa shule za sekondari za serikali pamoja na maofisa elimu kwenye kikao cha kutathmini michango inayotolewa shuleni.

Alisema wakuu wa shule wanapaswa kuwapokea wanafunzi wote walichaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika mazingira yoyote waliyonayo hata kama watakuwa hawana michango.

Kadhalika, alisema waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano wawe wana michango au hawana kwa mazingira yoyote ni lazima wapokelewe na kinachohitajika ni kufahamu kuwa wamechaguliwa kujiunga na shule za serikali na sio vinginevyo.

"Tunapaswa kujiuliza michango sio kitu ambacho kinaathiri mshahara wa mwalimu au chakula cha mwanafunzi kwani tayari bajeti yake ilishapangwa na serikali, hivyo ni lazima tujielekeze kwenye vitu 'basic' (msingi) ndiyo vitolewe michango huku ni tofauti na shule binafsi ambako bila ada mwanafunzi haruhusiwi kufanya mtihani.

"Ni lazima tuangalie huu mzigo wa wazazi kwani watoto wengi walikuwa wanachaguliwa kujiunga na kidato cha tano, lakini hawana uwezo Rais Samia Suluhu Hassan ameondoa ada sasa na sisi hii michango inabidi kuiangalia ili kubakiza vitu vya msingi na isizidi shilingi 150,000," alisisitiza Mtaka.

Pia alipiga marufuku wanafunzi kulazimishwa kununua mahitaji yao kwenye maduka ya shule.

"Juzi mheshimiwa waziri wa fedha alikuwa anasema kwenye suala la manunuzi kwamba watoto wanaambiwa kununua track-suit shuleni kwa Sh. 50,000 ambayo angenunua hapa Dodoma barabara ya nane kwa Sh. 18,000, kwanini usimwache anunue, ila mwambie tunataka ya rangi ya bahari na hata kama akikosea rangi isiwe sababu ya kumfanya asirudi.

"Kwasababu kilichompeleka pale ni ufaulu wake wa darasani lazima tujielekeze kwenye mambo ya msingi tusiwe na duka la shule linalomkomoa mwanafunzi lazima tufahamu kuwa kila mtoto ana maisha yake na hizi ni shule za umma," alionya.




Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Juma Kimori (kushoto), akibadilishana mkataba na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Dk. Benson Ndiege, baada ya hafla ya kusaini makubaliano hayo kati ya ofisi ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na NMB wa kujenga maghala kwenye vyama vya ushirika, jana jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TCDC yavitaka vyama ushirika kuweka juhudi

**Na Gwamaka Alipipi**

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imevitaka vyama vya ushirika nchini kuweka juhudi ili kufanikisha sekta ya kilimo inapiga hatua.

Rai hiyo imetolewa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara, Dk. Benson Ndiege, akieleza kuwa serikali imetenga bajeti kubwa kwenye kilimo kwa mwaka ujao.

Alisema bajeti hiyo inatarajiwa kwenda kuimarisha katika ujenzi wa miundombinu ya kilimo kama vile umwagiliaji, uzalishaji, utumiaji wa mbegu bora na mbolea.

Dk. Ndiege alisema ili kufikia lengo la bajeti, vyama vya ushirika ni lazima vitekeleze jukumu lao la msingi la kuratibu na kuwasimamia wakulima.

Akielezea kuhusu umuhimu wa nafasi ya vyama vya ushirika, Dk. Ndiege alisema kwa kuwa bajeti ya kilimo imejielekeza katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, vyama vya ushirika vitakuwa ni chombo muhimu katika kusimamia na kuratibu wakulima, ili wamwagilie kwa utaratibu mzuri.

"Ili miundombinu hiyo iwe endelevu, ni lazima uwasimamie wakulima. Ni lazima uwe na mfumo wa kuwasimamia ili watumie miundombinu hiyo vizuri," alisema Dk. Ndiege.

Alisema kuwa bajeti ya mwaka ujao inatarajiwa kuongeza uzalishaji katika kilimo, hali ambayo itahitaji masoko zaidi vyama vya ushirika vitahitajika kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika.

Alisema wiki iliyopita TCDC ilisaini mkataba na Benki ya NMB wa Sh. bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya mazao kwa vyama vya ushirika nchini.

Alisema ujenzi wa maghala hayo utasaidia kuongeza uhifadhi na masoko kwa wakulima.

"Kwa vile inategemewa kuwa bajeti itaongeza uzalishaji katika kilimo, makubaliano hayo yanatarajiwa kuokoa mazao yanayopotea kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhi," alisema Dk. Ndiege.

Dk. Ndiege alisema kutokana na matatizo ya kukosekana kwa maghala, serikali kupitia Tume ya Ushirika iliona ni muhimu kukaa na NMB na kujadili namna ya kutatua matatizo hayo.

# Wanasaikolojia wataka kutambuliwa

**Na Mary Geofrey**

CHAMA cha Wanasaikolojia Tanzania (TAPA), kimedai kada hiyo imeendelea kutafsiriwa kama sehemu ndogo ya taaluma iliyomo kwenye ustawi wa jamii, kinyume na taratibu.

Hayo yalielezwa juzi mkoani Dar es Salaam na Rais wa chama hicho, aliyemaliza muda wake, Atuwene Mbele, kwenye mkutano mkuu wa sita wa TAPA, ambao ulifanya uchaguzi kuwapata viongozi wa juu wapya.

Atuwene alisema, kwa kipindi cha karibuni wanasaikolojia nchini wamehusishwa kwenye mijadala tofauti, ikiwamo bungeni, ingawa umuhimu wao bado haujapewa kipaumbele.

"Lengo la umoja huu ni kuwa pamoja, kutambuana. Taaluma hii imevamiwa na vishoka watu wanajiita wanasaikolojia na kutoa tiba sahihi kwa jamii, lawama tunatupiwa wote, sababu hatuna bodi," alisema Atuwene.

Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge wa Ubungo, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alisema mahitaji ya wanasaikolojia yanaongezeka licha ya jamii kutoyatambua majukumu yao kwa usahihi.

"Saikolojia ni kuwapa watu furaha kuepukana na huzuni. Maisha ya binadamu huzuni iwe ni muda mchache, unaweza ukazungumza na mtu ambaye angeenda kujiua, lakini elimu yako ikamjibu na kumzuia kutenda hivyo," alisema Prof. Kitila.

Awali, Katibu Mkuu TAPA, Magolanga Shagembe, ambaye aliteuliwa kuwa rais wa chama hicho, alisema wanasaikolojia wafuate maadili kinyume chake ni kutoitendea haki taaluma na jamii.

"Tuhakikishe tunayafuata maadili, yawe na thamani, uwe mwema kwa jamii, usifanye kitu usicho na ujuzi nacho, ukiona ushauri ulioumpa mteja wako haujatosha, mpe rufani kwa walio juu yako, ili kuiponya jamii," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF izisaidie klabu CAF kwa Ligi Kuu kuanza mapema

**BINGWA** wa Ligi Kuu Tanzania Bara tayari ameshajulikana wakati msimu huu wa 2021/22 ukielekea ukingoni ambapo Klabu ya Yanga imefanikiwa kutwaa taji hilo kabla ya msimu kumalizika rasmi Juni 29, mwaka huu.

Kwa maana hiyo, Yanga ina tiketi mkononi ya kuiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Simba ambayo imejihakikishia kumaliza katika nafasi ya pili msimu huu kutokana na kufikisha alama 54 ambazo haziwezi kufikiwa na timu nyingine.

Ikumbukwe msimu ujao, Tanzania inaingiza timu nne kwenye michuano ya kimatifa; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika.

Na kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), bingwa wa ligi hiyo na mshindi wa pili, watawakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati timu itakayomaliza nafasi ya tatu na itakayotwaa Kombe la FA, zikikata tiketi ya kupeperusha bendera ya Tanzania Kombe la Shirikisho Afrika.

Lakini, kama bingwa wa Ligi Kuu ndiye atakayetwaa Kombe la FA, basi timu itakayoiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika itakuwa ni ile itakayomaliza nafasi ya nne kwenye Ligi Kuu ambayo itaungana na iliyomaliza nafasi ya tatu.

Hivyo, kutokana na msimamo wa Ligi Kuu ulivyo, bado hakuna uhakika wa timu zitakazomaliza nafasi ya tatu na ya nne, huku pia fainali ya Kombe la FA kati ya Yanga na Coastal Union, ikitarajiwa kupigwa Julai 2, mwaka huu.

Hata hivyo, tayari Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limeshatangaza msimu mpya wa michuano yake hiyo, kwamba utaanza Agosti 12, mwaka huu kwa kupigwa mechi za awali. Hiyo ikimaanisha kutoka tarehe ambayo fainali ya Kombe la FA nchini, itapigwa zitakuwa zimebaki siku 40 tu kabla ya michuano hiyo ya CAF kuanza rasmi.

Kwa ujumla muda ni mchache sana wa maandalizi kwa wawakilishi wetu wa kimataifa, na kuna kila dalili kwa michuano hiyo kuanza kabla ya msimu mpya wa Ligi Kuu Bara kuanza jambo ambalo linaweza kuchangia timu zetu kushindwa kufanya vizuri.

Hii ni kutokana na kutambua wazi kwamba mwanzo wa msimu wachezaji wengi huanza kwa kujitafuta kwanza kwenye viwango vyao kabla ya kuanza kuchanganya baada ya mechi nne hadi sita, hiyo ikichangiwa hasa na kupata maandalizi duni ya msimu.

Tunasema hayo, hasa tukizingatia ligi imechelewa kumalizika, hivyo dirisha la usajili litachelewa kufunguliwa na kufungwa pia, jambo ambalo litachangia hata maandalizi ya msimu mpya (pre-season) kwa timu kuwa fupi.

Hivyo, TFF pamoja na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), hawana budi kuhakikisha kwanza dirisha la usajili linafunguliwa siku moja tu baada ya ligi kumalizika, lakini ikiwezekana kutangaza mapema msimu wa Ligi Kuu uanze Agosti Mosi, mwaka huu.

Kwa kufanya hivyo, kutawezesha wawakilishi wetu kujipanga na kujiandaa vema kuelekea michuano hiyo, ili kwenda kutoa ushindani wa kweli zaidi na si kuishia kuwa wasindikizaji kwa kushiriki tu.

Tunaamini kama ligi yetu itaanza mapema, kutatoa fursa pana kwa mabenchi ya ufundi ya wawakilishi wetu wa nchi kwenye michuano hiyo kurekebisha makosa huku kukisaidia wachezaji wao kurejea mchezoni haraka zaidi katika mechi za kimashindano.

Madhumuni yetu ni kuona wawakilishi wetu wanakwenda kuipeperusha vema bendera ya Tanzania kwenye michuano hiyo, angalau timu itakayofanya vibaya iishie hatua ya makundi, huku malengo ya kila timu yakiwa ni kutinga nusu fainali na kuendelea kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wachezaji wa Kibongo mnakwama wapi?

Na Adam Fungamwango

**KWA** misimu kadhaa sasa kila ukija wakati wa dirisha la usajili wa wachezaji, neema inaangukia zaidi kwa wachezaji kutoka nje ya nchi na si wazawa.

Klabu kubwa kama Simba, Yanga na Azam zinakuwa zikipigana vikumbo kusaka wachezaji wa kigeni kwenye mataifa mbalimbali.

Siku hizi utakuta klabu hizo zikipigana vikumbo kwenda kusajili mpaka wachezaji kutoka Rwanda, na Burundi ambapo kwa miaka ya 1980, ilikuwa si tu ni aghalabu, ila haiwezekani.

Ni kwamba wakati huo Tanzania ilikuwa na wachezaji wengi wenye vipaji kuliko Rwanda na Burundi. Wachezaji wa Tanzania walishindana kwa ubora na wachezaji wa Zambia, Kenya, Uganda, Malawi, Nigeria, Guinea, Zaire (sasa DRC) na Ghana.

Kadri misimu inavyozidi kusonga mbele, binafsi nilianza kuhisi kuna kitu kitatokea mbele ya safari na kweli kimeanza na huko tunakokwenda msimu ijayo itakuwa ni hatari zaidi.

Nilianza kuona taratibu klabu kubwa na zenye uwezo kipesa kama Simba, Yanga na Azam zinakuwa zikiangalia zaidi wachezaji wa kigeni na si wa Kitanzania kwa jili ya kuunda timu zao.

Inavyoonekana zimeshaona ili ziwe na msingi mzuri ni lazima zisajili wachezaji wa kigeni, na baadaye kusajili wazawa kama vile kuongezea, au kutimiza idadi inayotakiwa ya wachezaji kuanzia 25 hadi 30.

Nadhani wakati mwingine kuna timu zinasajili wachezaji wa Kitanzania kwa sababu tu ni lazima wasajiliwe, yaani kuna idadi ya mwisho iliyowekwa ya wachezaji wa kigeni, la sivyo kama wangeruhusiwa basi ama wangesajili wote wageni, au wazawa wasiozidi watano tu.

Huko nyuma klabu za Simba na Yanga zilikuwa zikigombea wachezaji wazawa hapa hapa nchini, lakini sasa zimegeuka, zinagombea wageni.

Kumbuka zilivyokuwa zikiwagombea kina Malimi Busungu, Said Bahanuzi, Ramadhani Singano, Kelvin Yondani, na wengineo, lakini kadri misimu ilivyozidi kusonga mbele hali ikazidi kubadilika.

Mfano mzuri msimu huu, Yanga imetangaza kuwa itasajili wachezaji wasiozidi au kupungua wanne wa kigeni tu basi.

Ina maana kwenye usajili msimu huu wa Yanga wachezaji wa Kibongo hakuna mwenye nafasi ya kusajiliwa. Pamoja na jitihada zao zote za kucheza soka kwenye klabu mbalimbali ili waonekane, lakini nafasi hakuna.

Kwa sasa nafasi ipo za Simba na Azam tu kwenye klabu zenye pesa nzuri, ambako hata huko nako nina uhakika kuna nafasi chache sana za wazawa. Kama hali ikiendelea hivi, kuna msimu unaweza kukuta Simba, Yanga na Azam zote hazitosajili mchezaji yeyote wa Kibongo.

Viongozi wa klabu hizi wanafanya makusudi? Hapana, ni kwa sababu wanaona hakuna wachezaji wa viwango ambavyo wanavihitaji kwenye timu zao.

Pamoja na kudaiwa kuwa ligi imekuwa ngumu na wachezaji wamejituma sana msimu huu, lakini bado hakuna viwango vya wachezaji wengi wa Kitanzania ambavyo vingeshawishi klabu hizi kushtuka.

Hata huyo George Mpole ambaye amekuwa na msimu mzuri, bado ni kama vile klabu hizo zina mashaka naye, kwani wachezaji wa Kibongo wameonekana ni kama maji kubwa na kujaa, msimu huu anaweza kucheza hivi na msimu ujao vile.

Nasikia Simba wanamnyemelea, na hii ni kwa sababu tu msimu huu wataondoka mastraika wengi kutokana na kuonekana kushuka viwango, vinginevyo hata huko asingepata nafasi.

Yanga ilifanya usajili kipindi cha dirisha dogo kwa kuwachukuwa, Denis Nkane kutoka Biashara United na Chrispin Ngushi, kutoka Mbeya Kwanza waliokuwa wanafanya vema, lakini mpaka sasa hakuna maajabu makubwa waliyofanya, cha maana wakiwa huko. Mchezaji pekee ambaye ameonyesha mafanikio ni Salum Aboubakar 'Sure Boy'.

Hii inaonyesha kuwa bado wachezaji wa Kitanzania wana safari ndefu sana na inabidi wajiulize wanakwama wapi?

Yupo shabiki mmoja alisema Taifa Stars haifanyi vema kwa sababu Ligi Kuu ya Tanzania ina wachezaji wengi wageni. Mwenzake akamjibu mbona timu ya Algeria nayo haina wachezaji wa Ligi Kuu ya Algeria? Swali lake likafa hapo hapo. Ina maana Algeria ilitumia wachezaji wengi kutoka nje ya nchi.

Hivyo, ufumbuzi wa ubishi wao ukawa wachezaji wa Kitanzania nao watoke waende wakacheze soka nje ya nchi. Nasikitika kusema kama hapa kwenyewe Tanzania wengi wao si mhimili katika klabu zao hasa kubwa, unadhani kweli wengi wao wanaweza kucheza kwa mafanikio nje ya nchi?



Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Kennedy Nyoni (katikati), akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Absa Tanzania, Abdi Mohamed (kulia) na Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, Mervin Saprapasen, katika uzinduzi wa kampeni ya uboreshaji wa huduma za kibenki kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (SME) uliofanyika jijini Dar es Salaam mwisho mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aweso azindua programu usimamizi maji

**Na Frank Monyo**

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amezindua programu ya uongozi wa maji duniani yenye lengo la kubadilishana uzoefu wa kimataifa wa namna ya bora ya kushirikisha na kuwahamasisha viongozi wa kisiasa na sekta mbalimbali katika usimamizi, utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini.

Alikuwa akifungua mkutano wa tano wa Jukwaa la Taifa la Wadau wa Sekta Mtambuka katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji katika Ukumbi wa Mikutano wa Benki Kuu ya Tanzania, jijini Dar es Salaam jana.

Aweso alisema kuwa thamani ya rasilimali za maji katika uchumi wa nchi ni kubwa kwa sekta zote ikiwamo kilimo, uvuvi, mifugo, nishati, ujenzi, uchukuzi, kuijua thamani ya maji pia itasaidia kubadilisha mtizamo wa wadau na kuweka mikakati ya pamoja ya utunzaji na uendelezaji wa rasilimali za maji.

Aliwataka wadau hao kutumia jukwaa hilo kutafakari na kujifunza kutoka nchi nyingine na kujiweka tayari kufanya tathmini ya kina kujua thamani ya maji nchini na kujadili kupata namna bora ya kufanya tathmini hiyo.

Alisema anatarajia jukwaa hilo litachochea na kuongeza maarifa na weledi katika utafiti na tathmini za rasilimali za maji, ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kama mabwawa na kuongeza ufanisi wa maji hususani kwenye kilimo.

"Tathmini ya wizara ya hivi karibuni inaonesha rasilimali za maji zinazoweza kupatikana kwa mwaka kwa matumizi mbalimbali nchini ni wastani wa mita za ujazo bilioni 126.

Alisema kuwa kiasi hicho zaidi ya mita za ujazo 1,700 ni cha chini cha mahitaji ya maji kwa mtu kwa mwaka kinachokubalika kimataifa.

Aweso alisema maji ni msingi wa maendeleo na kichocheo kikubwa katika kukuza uchumi nchini kwa rasilimali za maji zinasaidia kukuza uchumi kupitia shughuli mbalimbali.

Pia, alieleza nchi inatekeleza dira na sera ya viwanda ambayo inategemea upatikanaji wa umeme wa hakika na gharama nafuu na taarifa za wataalamu zinaonyesha gharama za uzalishaji umeme kwa nguvu za maji ni nafuu kuliko wa gesi asilia na mafuta ya dizeli.

"Sekta ya maji imebadilika sana ndani ya muda mfupi, kwa sababu tulikuwa na miradi kichefuchefu 177 ambayo ilikuwa ikilalamikiwa na wananchi, lakini tumefanikiwa kuitatua 126 hadi sasa," alisema.

Aliahidi kwa wadau hao kuwa kwa mwaka ujao atakuwa kiongozi wa kwanza kusimamia rasilimali za maji nchini kwa kufanya ziara za kimkakati katika kila bonde la maji ili kuwezesha kila mtu kuzifahamu na kuzitunza rasilimali hizo.

# 'Panya Kaloa' wadaiwa kupora, kukaba

**Na Mwandishi Wetu,**

DODOMA

KUNDI la kihalifu linalojiita 'Panya Kaloa', limetajwa kuwa tishio katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Dodoma, huku Jeshi la Polisi likisema limewatia mbaroni vijana zaidi ya 20 wakituhumiwa kujihusisha na uhalifu wa kukaba na kupora watu. Mitaa inayotajwa kusumbuliwa na kundi hilo ni Msangalale, Kisasa, Tambukareli, Ilazo na Njedengwa, na kundi hilo limekuwa likipora wananchi, huku wengine kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwamo kubakwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao walidai kuwa vijana hao hutembea kwa kundi la watu wanne hadi sita wakiwa na vitu vyenye ncha kali, na kuwapora wananchi huku wakati mwingine wakivamia kwenye nyumba na kufanya uhalifu huo.

Mkazi wa Njedengwa West, Elizabeth Hobe, alisema vijana hao ni kikwazo kwenye mtaa huo na kuwafanya watu wakose amani.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Daimu Haji, akizungumza hivi karibuni, alisema kundi hilo huvamia sherehe wakiwa na mapanga, bisibisi na visu kisha hupora watu.

Mmoja wa waathirika, Neema Ndowe, aliiambia Nipashe kwamba alikabwa na vijana watatu ndani ya geti lake majira ya saa nne usiku na kumpora vitu mbalimbali.

"Hali sio nzuri, mimi tukio la kukabwa lilitokea Mei mwaka huu, hii hali bado naona tatizo. Mimi nilikabwa na vijana watatu na mapanga yao na ilikuwa saa nne kasoro usiku ndani ya geti yaani nilivyoingia ndani ile nataka kufunga geti wakawa wameingia ndani," alisema.

Alibainisha kuwa alitoa taarifa Kituo cha Polisi Kisasa, lakini wakati anafika kulikuwa na watu watatu wengine wakitoa taarifa hizo hizo za kukabwa kama ilivyomtokea yeye.

"Nilikuta kesi tatu za matukio kama haya nilivyosimulia na ilivyonikuta ndiyo kama wenzangu," alisema. Alipoulizwa Kamanda wa Polisi mkoani humo, Martin Otieno, alisema: "Wewe umesikia makundi ya hao panya kaloa katika wiki mbili zilizopita? Hakuna."

Alipoulizwa kuhusu waliokamatwa, Kamanda Otieno alisema: "Tulishatoa taarifa, zaidi ya vijana 20 wamekamatwa na wengine walishafikishwa mahakamani."

Alisema jeshi hilo linaendelea kuchukua hatua madhubuti za kukabiliana na uhalifu na kuwataka wazazi kuwadhibiti watoto wao ili wasifanye uhalifu. Juni 13, bungeni, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, akiuliza swali la nyongeza, kuhusu kuzuka vikundi vya uhalifu katika Kata ya Makulu Jiji la Dodoma vinavyojiita 'Panya kaloa' na kuhoji nini mkakati wa serikali ili kuvidhibiti vikundi hivyo kwenye maeneo mengine.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, alisema tayari polisi mkoani Dodoma wameanza kudhibiti vikundi hivyo na kuna vijana wametiwa nguvuni, huku akilihakikishia Bunge kuwa watawashughulikia hao panya kaloa.

# Waumini wasusia ibada, wadai kukuta wageni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BAADHI ya waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Ruanda jijini hapo, jana walisusia ibada iliyokuwa inaongozwa na Askofu mstaafu wa Dayosisi ya Konde, Dk. Izrael Mwakyolile, wakisisitiza ujio wake ni sawa na uvamizi.

Asubuhi waumini wa kanisa hilo, wafuasi wa aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Konde, Dk. Edward Mwaikali, waligoma kushiriki ibada hiyo baada ya kufika kanisani hapo na kukuta kanisa likiwa limejaa wageni na ibada ikiendelea.

Waumini hao walidai kugoma kuendelea na ibada hiyo baada ya kukuta gari la polisi lililokuwa na askari wenye silaha ndani, likizunguka nje ya kanisa, jambo walilosema hawajalizoea.

Mmoja wa waumini hao, Fabiola Kapinga, alisema walikuwa hawana taarifa yoyote kuhusu ujio wa wageni katika kanisa lao na wageni hao waliwaona kama wavamizi.

Alisema baada ya kufika kanisani walitegemea wangewakuta viongozi wao, lakini hakuwapo hata mmoja na badala yake waliwakuta wachungaji wapya na kwaya zilizokuwa zikiinjilisha zilikuwa ngeni.

"Hapa hatujamwona mchungaji wetu Mwambola wala Askofu Dk. Mwaikali, sasa tumeona ni vyema tukae nje maana hawa ni wavamizi ndani ya kanisa letu," alidai Fabiola.

Vilevile, alidai wachungaji wao wananyanyaswa hali inayowafanya washindwe kuendelea kuhubiriwa na watesi wa wachungaji hao na kushindwa kusikiliza vizuri neno la Mungu.

Naye Osia Manombo, alisema alipofika kanisani na kukuta gari ya polisi nje alidhani kuna mhalifu kanisani anayetakiwa kukamatwa, lakini alipouliza aliambiwa kanisani kuna wageni.

Alisema baada ya kuona hali hiyo alikosa amani na akaona vyema akae nje ya kanisa ili kujiweka salama kutokana na waliokuwamo kanisani kutokuwa waumini wa kanisa hilo hasa katika Usharika wa Ruanda.

"Lakini nimeuliza nikaambiwa kwamba kuna mabadiliko ya wachungaji, sisi tunawaamini wachungaji wetu na tunaamini kwamba wana Mungu wa kweli, sasa kwa kuletewa hawa wageni tena na magari ya polisi yako nje kwa kweli tumekosa amani," alisema Manombo.

Alisema ugomvi wa maaskofu hauwahusu waumini wa kawaida na kwa sasa kinachoendelea ni waumini hao kupandikizwa mgogoro ambao hauwahusu wao.

Alidai baadhi ya viongozi wa kanisa hilo wanalazimisha waumini hao kuingia kwenye taharuki ambazo hazina msingi na kuwaomba kuacha kugombana kama maandiko matakatifu yanavyowaelekeza wafatute amani na watu wote. Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Dk. Mwakyolile aliwataka wachungaji wote wa kanisa hilo kuungama na kutubu dhambi zao na kuwa wakati wote wa mgogoro walikoseana na kuwapoteza baadhi ya waumini.

Alisema baadhi ya waumini waliona ni bora waache kusali na wengine kuhamia kwenye madhehebu mengine wakiamini kwamba ndani ya kanisa hilo hakuna Mungu tena.

"Mkuu wa Kanisa la KKKT, Dk. Fredrick Shoo, ameniagiza nimfikishie salamu, anawapongeza kwa kuwa wastahimilivu katika kipindi chote cha mgogoro, anasema mlisimama imara kuanzia mwanzo mpaka mwisho, hongereni sana," alisema Dk. Mwakyolile.

Aliwataka waumini kuungana kwa pamoja na kuendelea kumtumikia Mungu badala ya kuendeleza migogoro ambayo alisema haina maana ndani ya kanisa.

# Wakazi 5,000 kutolipwa fidia upanuzi mgodi

**Na Faustine Feliciane**

MTHAMINI wa serikali, Rashid Mageta, amesema wakazi 5,000 wa Kijiji cha Komarera, Wilaya ya Tarime, mkoani Mara waliopaswa kupisha upanuzi wa shughuli za mgodi wa dhahabu wa Barrick North Mara, hawatalipwa fidia yoyote.

Amesema hatua hiyo imekuja baada ya kubainika wamejenga na kufanya shughuli za kilimo kwenye eneo lililozuiwa kisheria kuendelezwa.

Mageta aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kuwa wananchi hao walitegesha majengo na mashamba baada ya tangazo la serikali la zuio la kuendeleza eneo hilo kutolewa kwa mujibu wa sheria.

Awali, zaidi ya Sh. bilioni 20 zilikuwa zitumike kuwalipa fidia kabla ya kubainika udanganyifu wao.

Mageta alisema ujanja huo wa kutegesha ardhi kwa ajili ya kupata malipo ya fidia ulifanyika baada ya kutolewa tangazo la serikali kuzuia eneo hilo kutoendelezwa Mei, mwaka 2020.

Alisema watu 6,847 ambao madai yao ni halali kutokana na uthamini huo watalipwa Sh. bilioni 26 na tayari ulipaji umeshaanza.

Alisema hadi sasa wakazi 2,058 wamelipwa Sh. bilioni 8.9 huku zoezi la ulipaji likiendelea.

"Utathmini uliofanyika ni wa Sh. bilioni 46, lakini imebainika kuwa kati ya hizo, Sh. bilioni 20 ni 'tegesha', zingelipwa kwa watu wasiostahili, hivyo hawatalipwa," alisema. Mageta alisema, pia wenyeji wenye nyumba zilizoongezwa baada ya kutoka tangazo hilo nao hawatalipwa.

Alisema tangazo hilo la serikali lilitangazwa kwenye mkutano wa hadhara wa kijiji na kubandikwa kwenye ubao wa matangazo wa Ofisi ya Serikali ya Kijiji.

"Nyumba halali zitalipwa, lakini zilizoongezwa hazitalipwa. Picha za setilaiti zinaonyesha kila kitu kilichokuwapo wakati tangazo la katazo la kuendeleza eneo la mradi linatolewa," alisisitiza Mageta.

Alisema miongoni mwa mambo yanayozingatiwa wakati mgodi unahitaji eneo jipya kwa ajili ya shughuli za uchimbaji ni kufanya uhamasishaji kwa wananchi waliopo katika eneo husika.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Komarera, Nyamaganya Marwa, alikiri kuwapo kwa baadhi ya watu kujihusisha na vitendo vya kupanda miti katika eneo hilo.




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa TCB, Dk. Edmund Mndolwa (katikati), akitoa maelezo kwa waandishi wa habari (hawapo pichani), katika mkutano mkuu wa 30 wa wanahisa wa benki hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Wapili kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Njombe ajivunia tuzo ya mazingira

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, amewataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kutunza mazingira ili kuwa kinara. Mkoa huo ni moja ya mikoa mitatu nchini iliyopata tuzo ya utunzaji wa mazingira.

Kindamba, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akipokea tuzo maalum ya ushindi wa utunzaji wa mazingira, misitu na uoto wa asili iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia Muungano na Mazingira.

Kindamba alisema ulimwengu na mazingira yake mazuri sio kuwa umerithiwa kutoka kwa wazee bali umekopwa kutoka kwa watoto na vizazi vijavyo, kuna wajibu wa kuutunza ili kuhakikisha vizazi vijavyo vinakuta mazingira mazuri zaidi.

Alisema wachache wanao haribu mazingira wanapaswa kuendelea kupewa elimu kuwa uharibifu wa mazingira ni janga kubwa ambalo linaweza kuighharimu nchi siku za usoni.

Pia alimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, kwa kutambua kuwa Mkoa wa Njombe ni moja ya mkoa unaostahili kupata tuzo hiyo.

"Kwa niaba ya wananchi wa Njombe nimeipokea tuzo hii kwa mikono miwili na nitaitendea haki kwa kuhakikisha kwamba tunaendelea kutunza mazingira, vyanzo vya maji na maeneo teketeke ambayo kwa namna moja au nyingine yanafanya mkoa wetu uweze kung'aa katika utunzaji wa mazingira," alisema Kindamba.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Lulu Mussa, alisema mikoa ambayo imepata tuzo hiyo ni mitatu pekee hapa nchini ambayo ni Njombe, Katavi pamoja na Iringa.

Alisema tuzo hiyo imetolewa kwa Mkoa wa Njombe kutokana na kutambua mchango wa mkoa huo katika utunzaji wa mazingira na misitu kwa ujumla.

"Tunaamini tuzo hii itakuwa chachu kwa mkoa wako na mikoa mingine kuhamasika katika suala la utunzaji na uhifadhi wa mazingira," alisema Lulu.

Ofisa misitu na mratibu wa mazingira mkoani humo, Gumbo Mvanda, alisema katika mikakati ya kuhakikisha mazingira yanatunzwa zipo sheria ndogo zimetungwa za halmashauri kuhifadhi mazingira. Alisema ipo sheria mama inayotumika katika utunzaji wa mazingira ambayo ndani ya mita sitini kwenye vyanzo vya maji hakuna shughuli za kibinadamu kufanyika.

"Wananchi wa Mkoa wa Njombe wamekuwa mstari wa mbele hata kwenye masuala ya usafi kwani mara kadhaa halmashauri zetu zimekuwa zikipata ushindi kwenye mashindano mbalimbali ya kushindanisha masuala ya usafi na mazingira," alisema Mvanda.

# Fedha zatolewa kujenga vituo vitatu vya afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SERIKALI imeipatia Halmashauri ya Manispaa ya Singida Sh. bilioni 1.1 ujenzi wa vituo vitatu vya afya ili kuwasogezea karibu huduma wananchi.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Singida, Anwar Milulu, alisema hayo jana wakati wa mkutano wa wananchi wa Kata ya Mandewa ulioitishwa kuwaeleza maendeleo ya ujenzi wa kituo cha afya cha Mwaja katika kata hiyo.

Alisema fedha hizo zinazotolewa kwa awamu, zinaendelea katika ujenzi wa vituo vya afya vya Mtisi, Unyambwa na Mwaja na ujenzi utakapokamilika utaifanya manispaa kuwa na vituo vya afya vinne.

Utakapokamilika utapunguza kero ya wananchi kutembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata huduma za afya.

Milulu alisema katika kituo afya Mwaja ambacho serikali imetoa fedha nyingine Sh. milioni 250 na kufanya idadi fedha zilizotolewa kwa kituo hicho kufikia Sh. milioni 500, zitatumika kujenga wodi ya wazazi, operesheni na jengo la kufulia nguo.

Naye Kaimu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mandewa, Mwanahali Said, alisema ujenzi wa kituo cha afya Mwaja umefikia asilimia 90 na wananchi wanatoa ushirikiano kufanikisha ujenzi.

Alisema Sh. milioni 250 zilizotolewa zitakwenda kumalizia majengo yaliyobaki ambayo wana imani yanaweza kuchukua mwezi mmoja au zaidi kukamilika. Kwa upande wake Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Singida, Tumaini Sabbi, aliwataka wananchi wa kata hiyo waendelee kushirikiana na serikali katika ujenzi wa awamu ya pili ya kituo hicho.

"Maendeleo yataletwa na wananchi wenyewe kwa hiyo mhakikishe mnashiriki kwa moyo katika ujenzi kwa kujitolea na ulinzi wa kituo hiki cha afya ambacho ni cha kwenu," alisema.

Diwani wa Kata ya Mandewa, Baraka Hamis, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassani, kwa serikali yake kutoa fedha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya Mwaja ambacho kinakwenda kuondoa kero ya huduma za afya kwa wananchi wa kata hiyo na kata jirani.

Hamis alisema kabla ya kujengwa kwa kituo hicho wananchi walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma ya afya.

# Nipashe yasaidia mtoto mwenye kichwa kikubwa kupata msaada

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SHIRIKA la Child Help Tanzania (CHT) limesema litasaidia matibabu ya mtoto Collin Msambwa, mwenye umri wa miezi mitano, mkazi wa kijiji cha Kanikelele, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, aliyezaliwa na tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi hali iliyosababisha mama yake aamue kujinyonga.

Akizungumza kijijini hapo, Ofisa Habari Mawasiliano kutoka Shirika hilo, Milton Byemerwa, alisema baada ya kusoma taarifa iliyochapishwa na gazeti la Nipashe Juni 3, walifika kijijini hapo ili kuona namna watakavyosaidia kwa matibabu mtoto huyo na kutoa pole.

Alisema tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi sio uchawi bali ni ukosefu wa lishe kwa mjamzito.

"Jamii inapaswa kujua suala hili sio ushirikina, sio uchawi wala sio ulozi ni suala la kisayansi la mama kupata mimba au ujauzito akiwa na upungufu wa vitamini," alisema.

"Sisi tunashughulika na mtoto mwenye kichwa kikubwa na mgongo wazi kushauri kinga, lakini mtoto anapozaliwa na shida hiyo tunaweza kuelekeza mazazi kwenye hospitali za kibingwa zinazotoa huduma za kibingwa kama Moi, Bugando, Zanzibar ili mtoto aweze kupata matibabu," alisema.

Pia, alisema wanatoa vifaa tiba ambayo ni mirija ya kutoa maji kichwani kuyaingiza kwenye mfumo wa kawaida na vifaa vingine kama mirija ya kutoa haja kubwa na ndogo kwa watoto wasiokua na hisia.

Alisema watoto wenye mgongo wazi wanakosa hisia za haja kubwa na ndogo na ni maisha yao yote.

Vile vile, alisema kipo chama cha wazazi cha watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi na zaidi ya kaya 2,500 kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Zanzibar.

Babu wa mtoto huyo, John Lukelema alisema, analishukuru shirika hilo kwa kuonyesha jitihada za kumpatia matibabu mjukuu wake.

"Niwashukuru sana shirika hili maana kama hali yangu mnavyoiona sina uwezo nategemea kilimo, lakini nacho ni kigumu, nashukuru sana naomba mjukuu wangu apone kwa sababu tayari tuna madeni ambayo yalitokana na tulivyohangaikia tiba ya awali," alisema Lukelema.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Liganga, Roma Mhiche, alisema kuzaliwa mtoto mwenye changamoto kama hizo ni wa kwanza katika kitongoji hicho na watu walipokea tofauti.

"Kutokea kwa mtoto huyu kila mmoja alisema ni mtoto wa ajabu, nashukuru kwa msaada huu pia tutawaelimisha wanawake kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu," alisema Mhiche.



Mchambuzi wa Biashara wa Shell Natural Gas Series, Egejn Kiwia, akizungumza wakati wa kikao cha mnyororo wa thamani ya gesi asili kwa wanafunzi wa mwaka wa 1-4 wa shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kitengo cha migodi jiosayansi, kilichofanyika juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# MORUWASA yapewa bil. 1.5/- ujenzi matangi ya maji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), ili kufanya ujenzi wa matangi makubwa mawili ya kuhifadhi maji na kituo cha kusambazia maeneo ya Mkundi, Kihonda na Tungi.

Meneja Ufundi wa Moruwasa, Mhandisi Victor Ngowi, alisema hayo kwenye taarifa yake kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika manispaa hiyo ukiwamo ujenzi wa visima na kituo cha usambasaji maji.

Alisema, mradi huo ulianza kutekelezwa Machi 30, mwaka huu na umepangwa kukamilishwa Juni 30, mwaka huu unaolenga kutatua kero ya ukosefu wa maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

Ngowi alisema, ujenzi wa tangi kubwa la kuhifadhia maji upande wa Kihonda na Mkundi lenye ujazo wa lita milioni moja hadi kukamilika utagharimu Sh. milioni 600.

Meneja Ufundi wa Moruwasa alisema, upande wa Tungi na Kilimanjaro, ujenzi wa tangi utagharimu Sh. milioni 467, wakati ujenzi wa kituo cha pampu mbili za kusukuma maji utagharimu Sh. milioni 590.

Alimhakikishia Mkuu Mkoa kwamba, kwa pamoja mradi utakamilishwa kwa muda uliopangwa na watalazimika kufanya kazi hiyo usiku na mchana katika muda uliobaki ili kutumiza lengo lililokusudiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martin Shigela aliwataka maofisa wa Moruwasa na makandarasi wanaosimamia mradi huo kuwa unakamilika kwa wakati ili kutatua changamoto ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo.

"Serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa makandarasi, hivyo ninaagiza makandarasi na Moruwasa kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati ili ndani ya mwaka huu (2022), wananchi wa maeneo haya waanze kupata huduma ya maji," alisema Shigela.

Kwa upande wake Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga, aliishukuru serikali kwa jitihada za kutatua kero ya maji kwa wananchi wa maeneo hayo ya Mkundi, Kihonda na Tungi.

Alisema, maeneo hayo yanakabiliwa na changamoto ya maji na kimekuwa kilio cha muda mrefu kwa wananchi hao, kukamilika kwa miradi hiyo kutasaidia kuondokana na changamoto hiyo.

# Waonywa migogoro uongozi misikitini

**Na Shaban Njia**

WAUMINI wa dini ya Kiislamu Wilaya ya Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, wametahadharishwa migogoro ndani ya misitiki ya kugombania nafasi za uongozi.

Pia, wametakiwa kujikita katika kuwahamasisha waumini wao kushiriki sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agositi 23, mwaka huu.

Shekhe wa Wilaya ya Kigamboni, Abdallah Iddi, alitoa rai hiyo wakati wa ufunguzi wa Msikiti wa Jamiu Anwari, uliojengwa Kata ya Mji Mwema, Halmashauri ya Kigamboni kwa hisani ya watu wafanyao heri kutoka nchini Omani chini ya Jumuiya ya International Istiqaama.

Alisema, inapojengwa misikiti mipya nchini kumekuwa kukiibuka migogoro mikubwa ya kugombea nafasi za uongozi hali inayoleta taswira mbaya ndani ya uislamu na kuonya hatavumilia vitendo hivyo katika wilaya anayoiongoza.

"Sitakubali wala kusikia wilaya yangu hii inakuwa chanzo cha migogoro ndani ya nyumba za ibada, najua mnajua sina jeshi lolote ila nitamchukulia hatua za kisheria muumini yeyote atakayebainika kuwa chanzo cha migogoro ndani ya msikiti huu," alisisitiza Shekhe Iddi.

Alisema, kwa sasa kazi iliyoko ni kushirikiana na serikali kuwahamasisha waumini na wananchi wanaowazunguka kushiriki vyema sensa ya watu na makazi ili serikali ikamilishe azma yake kwa ajaili ya maendeleo ya wananchi wake.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kibugumo, Yusufu Tindwa alisema, itakuwa jambo la ajabu kama watabainika waumini wa dini ya kiislamu wanapinga na kuhamasisha watu wasishiriki sense.

Alifafanua kuwa sensa ilianza tangu kwa mitume wa Mungu waliotangulia na kwamba sio jambo jipya na kuwasisitiza kushiriki kwa pamoja.

Hata hivyo, alisema kabla ya kujengwa kwa msikiti huo, walifanya sensa kujua idadi ya waumini wa kiislamu waliopo eneo hilo, na hatajisikia vyema waumini watakapotajwa kuwa sehemu ya kukwamisha sense hiyo na atawawajibisha bila kujali dini wanazotoka.

Naye Diwani wa kata hiyo, Omary Ngulangwa, alisema ili kupata takwimu sahihi za wakazi inatakiwa kila mmoja kushiriki katika sensa kwa ajili ya maendeleo na kwa mtu atakayemficha mtu mwenye ulemavu atoe taarifa kwa viongozi waliopo jirani yake kwa hatua za kisheria.

Mmoja wa waumini wa eneo hilo, Mbwambo Omary alisema, anashukuru viongozi kuliona suala la migogoro ndani ya misikiti hali inayoleta mipasuko ya waumini kama yanavyoendelea katika madhehebu mengine.

Muumini mwingine Mwasiti Hamisi, alisema ili kufanikisha sensa kila mmoja anatakiwa kumhamasisha mwezake kama walivyokuwa wanahamasishana siku ya kwenda kupiga kura ya kuchagua viongozi wakati wa uchaguzi mkuu.

# Mahakama yatupa mashtaka uhujumu uchumi m'biashara

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam imetupilia mbali mashtaka 24 ya uhujumu uchumi yaliyofunguliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) dhidi ya mfanyabiashara, Jitesh Ladwa, yanayohusu kujipatia hisa 300 katika Kampuni ya Indian Ocean Hotels Limited.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ndimilanga, baada ya kuruhusu pingamizi la awali lililowasilishwa na mawakili Jeremiah Ntobesya na Juma Chuma, kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kuisikiliza kesi hiyo ambayo ina madai sawa na kesi ya madai inayoendelea Mahakama Kuu.

Hakimu Ndimilanga alisema kesi hiyo namba 28/ 2022 ilifunguliwa kinyume na marekebisho ya hivi karibuni ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), ambayo inakataza kufungua mashtaka ya kijinai kabla ya kumaliza kutafuta nafuu zilizoko kwanza kwenye madai.

Kutokana na hatua hiyo, Hakimu Ndimilanga aliamuru mfanyabiashara huyo kuachiwa huru.

Hata hivyo, baada ya kutoka mahakamani, mfanyabiashara huyo alikamatwa tena na askari na kupelekwa kwenye kituo cha polisi ambacho hakikujulikana.

Katika uamuzi wake, Hakimu Ndimilanga alibainisha kuwa mashtaka yaliyomo katika hati yanahusiana na mgogoro wa wanahisa katika kampuni binafsi isio na masilahi ya umma ambayo ipo katika Mahakama Kuu Kitengo cha Biashara Kanda ya Dar es Salaam.

Pia, Hakimu Ndimilanga alikubaliana na mawakili wa utetezi kuhusu sheria mbili za msingi, hususani kifungu cha 23 cha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Namba 1 ya mwaka 2022.

Mahakama ilitambua kuwa kulikuwa na kesi iliyoko Mahakama Kuu ya Tanzania (Divisheni ya Biashara) Namba 2 ya mwaka 2020, kati ya Chandulal Walji Ladwa na Dhirajlal Walji Ladwa, dhidi ya Jitesh Jayantilal Ladwa ya mgogoro wa hisa na wakurugenzi.

Miongoni mwa mashtaka yaliyofunguliwa na DPP dhidi ya mfanyabiashara huyo ni pamoja na kula njama ya kutenda kosa, kughushi nyaraka, kutoa nyaraka za uongo, kujipatia hati miliki kwa mikataba, kujipatia hisa kwa njia za uongo na kutakatisha fedha.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Joseph Sokoine, wakitiliana saini hati ya makubaliano baina ya Benki ya CRDB na wizara kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo wa kidigitali kwa Watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) jijini Dar Es Salaam, jumla ya Sh. milioni 100 zimetolewa na benki hiyo, kuwezesha mfumo wa kupata huduma mbalimbali wanazohitaji nchini wakiwa nje ya nchi. Mfumo huo utajumuisha watoa huduma wa serikali kama; NIDA, Uhamiaji na TIC. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NIT yatoa fursa zaidi wanafunzi 1,000

**Na Grace Gurisha**

CHUO cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), kimewapa fursa mbalimbali wanafunzi zaidi ya 1,000 wanaotarajia kumaliza masomo yao kwa kuwapa ufahamu wa mambo ya kufanya baada ya kumaliza ndani na nje ya nchi.

Ufahamu huo ulitolewa juzi na walimu wenye fani mbalimbali, wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Umahiri wa Kikanda upande wa Usalama Barabarani, Dk. Omari Mashi, akimwakilisha Makamu Mkuu wa chuo upande wa Taaluma na Ushauri Elekezi.

Akizungumza katika programu hiyo, Mashi alisema, wamewaita vijana hao kwa ajili ya kuwapa ufahamu kuhusu fursa mbalimbali zinazopatikana chuoni hapo au sehemu nyingine ndani ya nchi au nje.

Alisema jambo hilo hawakuwahi kulifanya, lakini wameona kuna muhimu kwa sababu wanapoingia chuoni wanaelekeza jinsi ya kuendeleza maisha yao na programu hiyo itawezesha kupata fursa mbalimbali.

"Waliyokuwa na hamu ya kuchukua programu zingine kama master's degree na postgraduate tunawaeleza nini cha kufanya na pia wanaoona wamefikia mwisho wanataka kufanya kazi tunawapa fursa za kazi," alisema Dk. Mashi.

Alisema chuo chao kina mchango mkubwa kuisaidia serikali suala la ajira kwa sababu wanajitahidi kufanya uhusiano au mawasiliano na vyanzo mbalimbali vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi kupata ajira.

Alisema wanashirikiana na taasisi na viwanda mbalimbali ambako wanafunzi wao huwapeleka kwanza kwenye mafunzo kwa vitendo, kwa baadaye wanapata fursa ya kuajiriwa kutokana na uhusiano walionao.

Kadhalika huwaalika wadau mbalimbali katika mahafali na kuwapatia wanafunzi ajira na limefanikiwa kwa sababu wengine anatoa zawadi kwa waliofanya vizuri.

"Hata hivyo, walimu wetu pia wamekuwa na mahusiano mazuri na wanafunzi pale inapotokea fursa huwa wanawatafuta kwa njia ya simu na pia hata hapa chuoni wanafunzi wanaofanya vizuri huwa wanabakishwa," alisema.

Mkurugenzi wa Research Publication and Postgraduate Studies (DRPPS), Dk. Eva Luwavi, aliwaeleza wanafunzi hao kuwa elimu waliyoipata haitoshi wanatakiwa waendelee kusoma.

"Lazima muongeze elimu hii haitoshi maisha yamebadilika sio kama zamani, zamani wazazi wetu walikuwa wanaona ukipata shahada ya kwanza ndiyo umemaliza, lakini kwa sasa haitoshi," alisema Dk. Luwavi.

Naye, mlezi wa wanafunzi kutoka Idara ya Ustawi wa Wanafunzi, Meshack Kimaro, aliwataka wanafunzi wenzake waende wakaishi kama watu waliyoelimika na wenye maadili na tabia njema walizotokanazo NIT.

"Huko mnakoenda mkayaendeleze mema mliyotokanayo NIT, muende mkaheshimike maisha bado yanaendelea, lakini chuo bado kiko nanyi kwa ushauri na mambo mengine," alisema.

# Singida yapania kuutokomeza ukatili kijinsia

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KAMPENI ya Shujaa wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA), Mkoa wa Singida imedhamiria kuwafikiwa wananchi 400,000 ili kuwapa elimu ya namna ya kupinga na kuufuta kabisa ukatili wa unyanyasaji wa kijinsia unaoikumba jamii nchini.

Kaimu Katibu wa SMAUJATA Mkoa wa Singida, Emanuel Digha, akizungumza katika mkutano wa wananchi wa kata ya Mandewa uliofanyika mtaa wa Mwaja, alisema watu hao watafikiwa katika kipindi cha ndani ya miezi mitatu hadi minne ijayo.

Alisema mbinu zinazotumika kutoa elimu ni kuhudhuria mikutano ya hadhara, kutembelea shule, kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamiii na wananchi wanapaswa kuunga mkono kampeni hiyo ili kukomesha vitendo vya ukatili.

Digha alisema vitendo vya ukatili vingi vinatokana na uelewa mdogo wa jamii na baadhi wamekuwa wakidanganywa na waganga wa kienyeji kwamba wakifanya jambo fulani la ukatili pengine watapata utajiri hali inayohusishwa na imani potofu.

Alisema ili kuhakikisha elimu ya kupinga ukatili inawafikia kwa uharaka jamii, SMAUJATA ipo mbioni kupata viongozi kuanzia ngazi za mitaa, vitongoji na vijiji ambao watakuwa na jukumu la kuwaelimisha wananchi kuachana na vitendo vya ukatili.

"Nawaasa wananchi vitendo vya ukatili sio vizuri maana sisi tumepewa maisha bure na Mungu kwa hiyo tuache ukatili ili kila mtu aishi na kufanya kazi zake kwa uhuru," alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa SMAUJATA mkoani hapa, Ambwene Kajula, alisema kampeni hiyo imekuja wakati mwafaka kutokana na makundi mengi kukumbana na ukatili na kuogopa kutoa taarifa ikiwamo kundi la watoto na wazee ambao mara nyingine hukatiliwa kutokana na imani potofu kama kuhisiwa na vitendo vya ushirikina.

"Nawasihi hata wanaume ambao hupigwa na wake zao, lakini wamekuwa hawasemi, hivyo basi kupitia kampeni hii tukishirikiana kutoa taarifa itakuwa msaada mkubwa sana," alisema.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa SMAUJATA Mkoa wa Singida, Vicent Mafuru, alisema kuwa watafikia Mkoa wa Singida kuanzia ngazi ya halmashauri, kata, vitongoji hadi vijiji na mitaa ili kutoa elimu na misaada mbalimbali ya namna ya kukabiliana na ukatili wa kijinsi ili kulifanya Taifa la Tanzania kuwa endelevu katika nyanja zote za kijamiii na kiuchumi.

Mafuru alisema jamiii mkoani hapa inatakiwa kutoa taarifa zinazohusu ukatili dhidi yao hasa wakati huu wa utekelezaji wa kampeni ya kupinga ukatilii.

"Wanajamiii wanatakiwa kutoa taarifa za matendo maovu yanayoendelea katika nyumba zao, shuleni na maeneo yote ambayo watu wanakumbana na kaadhia ya unyanyasaji na ukatili kwa kupiga namba 116 na atapata msaada, " alisema Mafuru.

NIPASHE JUMATATU JUNI 20, 2022
Nipashe
Spotika



MABEKI WA5 WA KATI WENYE THAMANI ZAIDI DUNIANI 2022 UK. 12



Salah
Nunez
Klopp

# SABABU 3 KWA NINI NUNEZ ATAFANIKIWA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, Uingereza**

KLABU ya Liverpool imefanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Benfica, Darwin Nunez kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 85, huku mshambuliaji huyo wa Uruguay akisaini mkataba wa miaka sita.

Nunez atavaa jezi namba 27 pale Anfield, ambayo iliachwa na Divock Origi msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, aliifungia Benfica mara 34 katika michuano yote msimu uliopita, ikiwa ni pamoja na mabao katika mechi zote za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool, Aprili mwaka huu.

Nunez amejidhihirisha kuwa miongoni mwa washambuliaji wa kutumainiwa zaidi barani Ulaya baada ya kuwa na msimu wa kuvutia wa 2021-22 akiwa na Benfica.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alifunga mabao 26 katika mechi 28 za ligi msimu uliopita. Pia alifunga mara sita katika mechi 10 za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Baada ya 'Wekundu' hao wa Anfield kukamilisha usajili huo, hapa tunaangalia sababu tatu kwa nini, Nunez atafanikiwa sana pale Liverpool.

**#1. Umri mdogo**

Kwa kawaida wachezaji wanakuwa bora kutokana na uzoefu na, akiwa na umri wa miaka 22, Darwin Nunez bado hajaingia kwenye ubora wa maisha yake ya soka. Huku makocha na wachezaji wa hali ya juu wakimzunguka, Nunez anaweza kuwa na nafasi kubwa zaidi ya kuimarisha kipaji chake pale Anfield.

Nunez alicheza mechi yake ya kwanza ya kulipwa akiwa na umri wa miaka 18, katika klabu ya Penarol mwaka 2017. Aliichezea klabu yake hiyo ya utotoni michezo 14 kabla ya kujiunga na Almeria ya Hispania mwaka 2019. Alitumia msimu mmoja pekee katika klabu hiyo yenye maskani yake Andalusia na akajiunga na Benfica mwaka 2020. Nunez amekuwa akiitumikia klabu hiyo ya Ureno tangu wakati huo.

Licha ya kuwa mdogo, Nunez ana uzoefu wa kucheza zaidi ya michezo 130 ya timu ya wakubwa na atakuwa na nafasi nzuri zaidi kwenye maisha yake ya soka pale Anfield. Inaweza kusemwa kuwa Wekundu hao wamemsajili Nunez kwa wakati ufaao, ikizingatiwa ubora wake bado unakuja.

**#2. Mstari wa straika bora ya Liverpool**

Liverpool kwa sasa wanamiliki moja ya mstari wa safu bora zaidi ya ushambuliaji katika soka la Ulaya. Kuondoka kwa Sadio Mane hivi karibuni kutawaacha Wekundu hao na Mohamed Salah, Diogo Jota, Roberto Firmino, Luiz Dias, na Takumi Minamino wakiwa washambuliaji wakuu.

Wekundu hao walifunga mabao 92 katika mechi 38 za Ligi Kuu msimu uliopita - wakishika nafasi ya pili kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi, nyuma ya mabingwa Manchester City. Ikizingatiwa kuwa Nunez sasa atakuwa miongoni mwa safu hiyo, Liverpool wanaweza kuwa hatari zaidi mbele ya lango la timu pinzani.

Raia huyo wa Uruguay alifunga asilimia 30.6 ya nafasi zake alizopata msimu uliopita, hivyo ni miongoni mwa wachezaji waliopiga mashuti 99 au zaidi langoni kwenye Ligi Kuu ya Ureno, Liga Bwin.

**#3. Mabeki wa pembeni wa Liverpool**

Mabeki wa pembeni wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold na Andy Robertson ndio wachezaji wabunifu zaidi kwenye Ligi Kuu England. Walisaidia mabao 12 na walifunga mabao 10 kwa ujumla kwenye ligi msimu uliopita.

Wawili hao hutoa pasi muhimu zaidi ndani ya eneo la yadi 18, ambayo ni ndoto nzuri kwa wachezaji wamaliziaji wazuri kama Nunez ambaye anaweza kufunga kwa miguu yote miwili au kwa kichwa.

Na kutokana na uwezo wake, anaweza kufunga mabao mengi zaidi hapo Liverpool kwa msaada wa mabeki hao wa pembeni.

## ISIKUPITE

HAWA ndio wachezaji bora wa msimu wa kila klabu katika klabu 6-bora za Ligi Kuu England msimu uliomalizika wa 2021-22; Manchester City (Kevin De Bruyne), Liverpool (Mohamed Salah), Chelsea (Mason Mount), Tottenham Hotspur (Son Heung-min), Arsenal (Bukayo Saka) na Manchester United (Cristiano Ronaldo).



## Extra Time



Ruben Dias, akiwa kazini

# MABEKI WA5 WA KATI WENYE THAMANI ZAIDI DUNIANI 2022

**LONDON, England**

MAJUKUMU ya mlinzi wa kati yamebadilika sana kwa miaka mingi sasa. Hapo awali, walikuwa na jukumu la kuwazuia washambuliaji wa upinzani kwa njia yoyote muhimu wasifunge mabao. Leo, wamepewa majukumu ya ziada kama vile umiliki na usambazaji wa mpira. Kuchanganya upinzani wa kuzuia mashambulizi kwa staili ya uchezaji wa zamani inakuwa kazi ngumu zaidi katika majukumu ya sasa ya mlinzi wa kati.

Ni mabeki wachache sana wa kati wanaoweza kufanikisha hilo, huku wengi wakishindwa katika eneo moja au jingine. Lakini wale wanaofanya wana thamani na uzito wao katika soko la leo.

Kwa mujibu wa utafiti wa Taasisi ya CIES Football Observatory. Hapa tutawaangalia mabeki watano wa kati walio katika kiwango bora zaidi duniani ambao ndio wenye thamani kubwa zaidi duniani kwa sasa...

**#5. Dayot Upamecano (Bayern Munich): Euro Milioni 77.7**

Bayern Munich walitumia euro milioni 42.5 kumsajili beki wa kati, Dayot Upamecano kutoka RB Leipzig msimu wa majira ya joto wa 2021. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, amehalalisha bei yake, na kuibua msururu wa maonyesho ya kuvutia kwa 'Bavaria' hao.

Beki huyo wa kati wa Ufaransa, anauwezo wa kumiliki mpira miguuni mwake, ana ustadi wa kusambaza pasi uwanjani.

Upamecano, ambaye kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 77.7, pia ni mbaya sana linapokuja suala la mtu na mtu.

Katika msimu wa 2021-22 wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Upamecano alishiriki katika michezo 28, akifunga bao moja na asisti sita.

Aliwasaidia hapo Bavaria kutoruhusu bao katika mechi nane za Ligi Kuu na nne kati ya nane za Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alikamilisha pasi 2048, akapiga pasi 10 muhimu. Alikoa hatari 33, na kuzuia mpira mara 69.

**#4. Ronaldo Araujo (Barcelona): Euro Milioni 89.1**

Barcelona hawakuwa na msimu mzuri zaidi wa 2021-22, huku wachezaji wao wengi wakihangaika kutimiza uwezo wao. Beki wa kati Ronald Araujo hakika hakuwa mmoja wao.

Alileta utulivu kwenye safu ya nyuma ya Barcelona na kusaidia timu yake kuendeleza mpira. Bila yeye 'Blaugrana' hao labda wasingeweza kushika nafasi ya pili.

Beki huyo wa kati wa Uruguay, ambaye thamani yake ni Euro milioni 89.1, alishiriki katika michezo 30 kwenye msimu wa La-Liga wa 2021-22, akifunga mara nne. Alikamilisha pasi 1485, alicheza pasi sita muhimu, na kutoa krosi mbili kwenye eneo la yadi 18.

Kwenye safu ya ulinzi, Araujo aliweza kudhibiti hatari 33, alizuia mikwaju 21, akavuruga mipango mara 37.

**#3. Eder Militao (Real Madrid): Euro Milioni 90.3**

Huku Sergio Ramos na Raphael Varane wote wakiondoka katika klabu kabla ya msimu wa 2021-22, Real Madrid ilihitaji mabeki kadhaa wa kati kujaza nafasi zao.

David Alaba na Eder Militao walikuwa kwenye nafasi nzuri zaidi kuwasaidia mabingwa hao wa LaLiga msimu wa 2021-22.

Beki wa kati wa Brazil, Militao alikuwa mmoja wa wachezaji walioiboresha zaidi safu ya nyuma ya 'Los Blancos' katika msimu wa 2021-22. Alikuwa mtu mahiri pale nyuma, alinasa mipira yote hatari, alionyesha upigaji wa pasi bora, na alikuwa akiupeleka mpira mbele kwa urahisi usioweza kufikiria.

Endapo Militao hangefanya vizuri kama alivyofanya, Real Madrid haingefanikiwa kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na LaLiga katika msimu wa 2021-22.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, ambaye thamani yake ni Euro milioni 90.3, alicheza mechi 34 za LaLiga msimu wa 2021-22, akiandikisha bao na kutoa pasi mbili za mabao. Militao amejidhihirisha kuwa ni beki mwenye tahadhari, akiokoa hatari 70 na kutoa pasi 125.

Beki huyo wa kati pia alikuwa na nafasi nzuri katika kusambaza mipira. Alikamilisha pasi 1779, alipiga pasi muhimu 11.

**#2. Josko Gvardiol (RB Leipzig): Euro Milioni 99.8**

Josko Gvardiol ndiye beki pekee wa kati kwenye orodha yetu leo ambaye hayumo katika klabu kubwa Ulaya. Lakini ikiwa beki huyo wa RB Leipzig ataendelea na uchezaji wake, anaweza kujikuta yupo kwenye moja ya klabu kubwa Ulaya hapo baadaye.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameibuka kama kitu kisichoweza kuhamishika kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, akiwavutia watazamaji kwa upigaji wa pasi zake nyingi, mbio za fujo, kulinda vizuri na usambazaji mzuri wa mipira.

Beki huyo mdogo wa kati raia wa Croatia, mara chache amehusika moja kwa moja mbele ya lango kwa sababu za wazi, lakini mtazamo wake wa mbele una jukumu muhimu katika mashambulizi ya Leipzig.

Gvardiol, ambaye thamani yake ni Euro milioni 99.8, alikuwa mmoja wa mabeki bora nchini Ujerumani katika msimu wa 2021-22. Ameshiriki katika mechi 29 za Bundesliga akiwa na Leipzig, akifunga mara mbili na kutoa pasi mbili za mabao.

Gvardiol alikamilisha pasi 1758 kati ya 2100 na alicheza pasi 11 muhimu. Beki huyo wa kati pia alicheza vema katika safu ya ulinzi, akizuia hatari 33.

**#1. Ruben Dias (Manchester City): Euro Milioni 109.6**

Manchester City ilimsajili Ruben Dias kwa ada ya Euro milioni 68 kutoka Benfica msimu wa majira ya joto wa 2020. Akiwa mlinzi ghali zaidi katika historia ya klabu hiyo.

Akiwa na kipaji, yeye, bila shaka, hakufanya makosa hata kidogo na alihalalisha bei yake ya juu katika msimu wake wa kwanza.

Akiweka utulivu katika safu ya nyuma ya City, aliisaidia timu hiyo ya kocha Pep Guardiola kuwa na kitengo cha ulinzi cha kutisha zaidi kwenye ligi.

Wakiwa njiani kuelekea kutwaa taji lao la Ligi Kuu msimu wa 2020-21, City waliruhusu mabao 32 pekee, idadi ndogo zaidi kwenye Ligi Kuu England.

Dias, ambaye ana thamani kubwa ya Euro milioni 109.6, ni mtengeneza pasi mzuri zaidi, na ni mahiri katika ujuzi wa mtu mmoja-mmoja.

Katika msimu uliomalizika hivi majuzi wa 2021-22, beki huyo wa kati alipiga pasi 2267, akitengeneza nafasi nne kubwa, alitoa pasi nne za mabao, na kufunga mara mbili.

Beki huyo wa kati wa Ureno pia aliisaidia timu yake kumaliza mechi bila kuruhusu bao ('clean sheets') mara 23 kwenye Ligi Kuu.

## Nukuu

"Ndio kuna timu nyingi, lakini nikiangalia viwango vya timu nyingine, Argentina na Brazil ziko juu zaidi na zina nafasi kubwa sana ya kufika fainali ya kubeba Kombe (la Dunia) mwaka huu. Kwa sasa nawaona kabisa Argentina na Brazil wakifanya makubwa kule Qatar hasa kutokana na aina ya wachezaji ilionao, ninawapa nafasi kubwa sana," **Kocha wa Hispania, Luis Enrique.**



"Mashabiki wanapaswa kuwa wavumilivu si kuanza kukosoa tu, ninaamini kwa ushirikiano na wenzangu, Simba inaweza kushinda ubingwa wa Afrika," **Straika mpya wa Simba, Mzambia Moses Phiri.**



"Mkataba wa [Kylian] Mbappe haukuleta shida yoyote na mpango wa [Erling] Haaland, kabisa. Tuna [Karim] Benzema, kwa hiyo hakuwezekana kuwa naye na Karim. Hatuwezi kumsajili Haaland kuja kukaa benchi. Haaland ni mchezaji wa ajabu na wa kushangaza, anastahili kucheza kila mechi," **Rais wa Real Madrid, Florentino Perez**



# AZIZI KI, NA MATUKIO MA5 YA UMAFIA SIMBA, YANGA

Na Adam Fungamwango

KILA inapofika nyakati za usajili nchini kunakuwa na hekaheka, habari nyingi, tetesi, stori za uongo na kweli, pamoja na kufanyiana umafia kunyang'anyana wachezaji, hasa kwenye klabu kongwe za Simba na Yanga.

Hii imekuwa kwa miaka mingi sana, Tanzania huwa kuna ligi mbili. Kwanza huwa na ligi ya uwanjani, lakini ikiisha wanachama na mashabiki wa soka wanakuwa roho juu kufuatilia mechi zao kujua ni nani atakuwa bingwa.

Ligi ikiisha huwa hawapumziki. Hapa kunakuwa na ligi kali sana kushinda hata ile ya uwanjani, nayo ni usajili na kikubwa zaidi kunyang'anyana wachezaji.

Kwanza kuna tabia ya kunyang'anyana wenyewe kwa wenyewe, kama tulivyowahi kuona kwa Ramadhani Waso, akitoka Simba kwenda Yanga, Kelvin Yondani akitoka Simba kwenda Yanga, Haruna Niyonzima akitoka Yanga kwenda Simba na hata misimu miwili iliyopita sakata la Bernard Morrison.

Kuna umafia mwingine ambao huwa zinafanyika kwa timu moja kumtaka mchezaji kutoka nje ya nchi, lakini kabla hawajakamilisha timu nyingine inakwenda kutibua mipango na kumchukuwa.

Imedaiwa hata Moses Phiri ambaye ametangazwa na Simba, Yanga tayari ilishapiga hodi huko ila 'ikadunda.'

Kwa sasa kuna sakata la mchezaji wa Asec Mimosas, Stephane Aziz Ki, ambapo timu hizo zinadaiwa kuvutana huku na huku kila mmoja ikimtaka, lakini mpaka sasa hakuna uhakika wa nani ameshaipata saini yake.

Kila mwaka huwa kuna usajili unatikisa, lakini msimu huu jina linaloonekana kutikisha kwenye vyombo vya habari ni Aziz Ki. Mwisho wa msimu itajulikana ataenda wapi, ingawa taarifa zinadai Yanga wapo kwenye hatua nzuri zaidi kuliko watani zao wa jadi, Simba.

Kutokana na tukio hili, katika makala haya tunakuletea umafia ambao timu hizi mbili zimewahi kuufanya kwa kunyang'anyana wachezaji. Mmoja anaongea naye, mwingine anakuja kumnyakua.




Stephane Aziz Ki

**#1. Bernard Mwalala - Yanga**

Anakumbukwa kuwa ni mmoja wa mastraika hatari, akicheza pia nafasi ya winga akitokea nchini Kenya. Baada ya michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati 2005 (Kagame Cup), kila shabiki wa soka alikuwa akimzungumzia mchezaji huyo wakati huo akiichezea SC Villa ya Uganda.

Kama kawaida Simba na Yanga zikaanza kampeni ya kutaka kumsajili. Vyombo vya habari navyo havikuwa nyuma, kuhabarisha umma juu ya timu hizo kumpata Ben Mwalala, straika mwenye kasi na uwezo wa kutupia.

Simba ilionekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumnasa kwa sababu ilionekana kuwa ndiyo wahitaji zaidi kuliko Yanga. Mashabiki wa Simba walijikuta na huzuni, zilipokuja habari kuwa ghafla kibao kimegeuka na Mwalala amejiunga na Yanga.

Na ndiye aliyefunga bao pekee la Yanga mwaka 2007 dhidi ya Simba, akifuta uteja wa misimu mitano Yanga kushindwa kuifunga Simba na kuichezea hadi 2009.

**#2. Mbuyu Twite - Yanga**

Ni sakata ambalo kwa miaka ya karibuni halijasahaulika na wanachana na mashabiki wa Simba kwa kuporwa mchezaji wao Mbuyu Twite akajiunga na Yanga kimaajabu.

Beki huyo wa kulia alikuwa amemalizana na Simba pamoja na kupewa pesa za usajili. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Simba wakati huo, Ismail Aden Rage, alimpa (dola za kimarekani 30,000). Akatambulishwa pia kwenye Simba Day ya 2012 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, ingawa hakuwapo.

Picha lilianza kugeuka pale Chama cha Soka Rwanda kushindwa kutoa Uhamisho wa Kimataifa (ITC). Tukio la kimafia likatokea, kwani zikaja taarifa kuwa Yanga nayo imemsajili. Hakuna aliyeamini.

Watu waliamini aliposhushwa nchini Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, akiwa na jezi ya njano na kijani, iliyoandikwa nyuma jina la 'Rage'. Simba ilikata rufaa Shirikisho la Soka nchini (TFF), lakini ilidunda, ilichoambulia ni kurudishiwa pesa dola 30,000 za Marekani.

Kilichobainika nyuma ya pazia ni kwamba inadaiwa mchezaji huyo alikuwa akicheza APR kwa mkopo, lakini ni mchezaji wa St Elio Lupopo ya Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, ambako Yanga ndiko ilikokwenda kumsajilia na kupata hati ya uhamisho. Mchezaji huyo aliichezea Yanga hadi 2017.

**#3. Laudit Mavugo - Simba**

Kulikuwa na vita kali kati ya Simba na Yanga kunyang'anyana mchezaji huyu wa Vital'O ya Burundi. Kuna kiongozi mmoja wa Yanga ambaye kwa sasa haypo, alikiri kuwa walimtaka straika huyo, lakini wakapinduliwa na Simba kutokana na uzembe mdogo uliofanyika.

Awali Simba ndio walioanza naye, lakini baadaye ikaonekana ni kama hawakuelewana, yakaisha. Yanga ikaingia kazini kuisaka saini yake. Lakini kabla mambo hayajakamilika, viongozi wa Simba wakarejea kwa kasi na kufanikiwa kumpata. Ni moja ya usajili uliokuwa gumzo nchini. Aliichezea Simba mwaka 2016 hadi 2018.

**#4. Meddie Kagere - Simba**

Yanga ndiyo ilikuwa klabu ya kwanza nchini kutaka kumsajili straika huyo ambaye yupo Simba mpaka sasa. Meneja wa mchezaji huyo, Patrick Gakumba, anathibitisha kwa kusema kuwa Kagere mwenyewe ndiye aliyeitolea nje na kuchagua kwenda Simba.

"Nilipokea ofa nyingi kwa timu tofauti zikimhitaji Kagere hata Yanga walileta, lakini mchezaji mwenyewe ndiye aliyekataa na akachagua kwenda Simba," alisema Gakumba.

Straika huyo raia wa Rwanda alikuwa akiichezea Gor Mahia wakati huo, alijiunga na Simba mwaka 2018 na hadi sasa yupo.

**#5. Luis Miquissone - Simba**

Kwa sasa anaichezea Al Ahly ya Misri, lakini alitokea klabu ya Simba. Winga huyo raia wa Msumbiji naye aliziingiza vitani Simba na Yanga zikapinduana.

Kwa mujibu wake mwenyewe kwenye mahojiano wakati yupo Simba, ni Yanga ndiyo iliyoanza kumfuatilia, lakini baadaye 'Wekundu wa Msimbazi' wakafanya umafia.

Alisema alianza kuongea na Simba, lakini walionekana hawakuwa na spidi, mpaka pale Yanga walipoingilia dili.

"Simba wakastukia kuwa Yanga wananihitaji, wakarudi kwa nguvu kubwa zaidi, kwani hata Yanga walipotuma mwakilishi wao hawakunikuta, Simba walinitumia tiketi ya ndege niondoke Msumbiji kwenda Afrika Kusini.

Baada ya kufika Afrika Kusini Yanga walikuwa wananipigia simu ambazo sikupokea kwani nilikuwa tayari huko nilikutana na kiongozi mmoja wa Simba, hakutaka kabisa niongee na Yanga, tukafanya mazungumzo ya kusaini mkataba yaliyochukua muda mrefu, lakini mwisho wa siku tulikubaliana nikasaini. Dili la Yanga lilikufa hapo hapo na ilibidi niwaambie ukweli ingawa hawakupenda kwani waliamini wangeweza kunipata kwa kuwa waliweka pesa nyingi kuliko zile za Simba. Baadaye nikagundua nilifanya chaguo sahihi kwangu kuliko Yanga pamoja na pesa zao nyingi," alisema Miquissone.

Je nani atashinda vita vya Aziz Ki? Hili nalo tusubiri tuone mwisho wake utakuwaje.

**JE, WAJUA?**



MLINDA mlango wa Real Madrid, Thibaut Courtois ndiye kipa bora zaidi kwa msimu wa uliomalizika wa 2021/22 akifuatiwa na Alisson Becker (Liverpool), Mike Maignan (AC Milan), Ederson Moraes (Manchester City) na Kevin Trapp wa Eintracht Frankfurt.



# Vitabu miongozo ya ufugaji vyazinduliwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amezindua vitabu vya miongozo ya ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji itakayosaidia wafugaji kufuga kisasa na kukuza kipato ili kujikwamua kiuchumi.

Uzinduzi huo umefanyika jana kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wafadhili wa mradi wa USAID/Lishe Endelevu.

Ndaki, alisema ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji ni muhimu kwa taifa, kwa sababu ni shughuli ya kiuchumi kwa ukanda wa Afrika kutokana na kuwa na tija katika kukuza kipato, kutengeneza ajira na kuboresha lishe ya wananchi.

Alisema ufugaji wa kuku ni njia mojawapo ya Watanzania kujitoa kwenye lindi la umaskini, kwa mujibu wa Sensa ya 2012 kuna wafugaji zaidi ya milioni nne wanaofuga kuku kuanzia 10 na kuendelea, ambayo ni sawa na asilimia 55.3 ya wafugaji wote.

"Ufugaji wa kuku, sungura na ukuzaji wa viumbe maji ni shughuli muhimu sana kwasasa katika nchi yetu na kwa uchumi wa wanachi wetu," alisema Ndaki.

"Wananchi wengi wanategemea ufugaji wa kuku ambao umezoeleka na kuku hao wanafugwa na kila mtu tofauti na nyuma watu walidhani ufugaji wa kuku unawahusu kinamama pekee," alisema.

Alisema ufugaji wa kuku na sungura ni njia mojawapo ya kuwatoa wananchi katika hali ya umaskini hasa waishio vijijini, uzinduzi wa miongozo hiyo umekuja wakati muafaka na kuitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kujipanga vyema kuisambaza katika kila ngazi kuanzia halmashauri hadi kata ili iweze kuwafikia walengwa.

"Tunatakiwa kuona ni namna gani tutahamasisha wafugaji ambao ni wanachi wetu ili waingie kwa nguvu kwenye ufugaji wa sungura kwa sababu ni chanzo cha lishe, lakini pia ni chanzo cha kipato kizuri," alisema Ndaki.

Hata hivyo, alisema wizara ikipata fedha katika mwaka ujao wa fedha watahakikisha wanalipa kipaumbele suala la ukuzaji wa viumbe maji.

Alisema tusiwe na hii miongozo halafu ikakaa kwetu tukabaki kuandika taarifa kwamba tumetengeneza miongozo kwa kushirikiana na wadau, lakini ipo kwenye makabati kinachotakiwa ni kuisambaza ili ikalete tija kwa wafugaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya USAID/ Lishe Endelevu, Dk. Joyceline Kaganda, alisema mradi huo ni wa miaka mitano unaofadhiliwa na USAID kwa msaada mkubwa wa watu wa Marekani, na kutekelezwa na Save the Children International na washiriki wake.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika mikoa minne ya Dodoma, Morogoro, Iringa na Rukwa na ulianza Oktoba 2018 hadi Septemba 2023.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza na walimu wakuu wa shule za sekondari za serikali (hawapo pichani), kwenye kikao cha tathmini ya michango inayotakiwa kutolewa shuleni kilichofanyika mkoani humo juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mchango chupa 550,000 damu salama wahitajika

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka wananchi kuendelea kuchangia damu ili kuokoa maisha ya watu na kufikia lengo la nchi kukusanya chupa 550,000 za damu ambazo ni mahitaji kwa mwaka 2022.

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Samwel Seseja, alibainisha hayo juzi wakati akihitimisha kampeni ya siku ya wachangiaji damu duniani iliyofanyika kikanda mkoani hapo.

Dk. Seseja alisema mpango wa taifa wa damu salama haujafikia lengo la kukusanya chupa za damu ambazo zinakidhi mahitaji ya nchi nzima.

"Ripoti ya mpango wa taifa wa damu imeonyesha katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kwa kushirikiana na timu za halmashauri wamekusanya chupa za damu 331,279 ambazo ni sawa na asilimia 88 ya lengo na asilimia 60 ya mahitaji ya nchi kwa kutumia vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) nchi inahitaji kukusanya damu asilimia moja ya wakazi wake au chupa 10 kwa kila wananchi 1,000 ambapo kwa Tanzania tumefikia chupa sita kwa kila wananchi 1,000," alisema Dk. Seseje.

Aidha, alisema upatikanaji wa damu ni muhimu kwa wagonjwa wenye uhitaji wakiwamo wajawazito, watoto kwa kuwa chupa moja ya damu inaweza kuokoa maisha ya watu watatu. "Siku ya Uchangiaji Damu ilianzishwa kwa dhumuni la kuongeza ufahamu wa hitaji la damu salama na bidhaa za damu kwa ajili ya wahitaji kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yamebeba kaulimbiu 'Kuchangia damu ni kitendo cha mshikamano tuungane kuokoa maisha'.

Meneja wa Damu Salama Kanda ya Kati, Dk. Katura Mathias, alisema mtu anayeweza kuchangia damu lazima awe ametimiza vigezo ikiwamo umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 65, uzito usiopungua kilo 50.

Alisema kwa mwanamke anapaswa asiwe mjamzito au anayenyonyesha na asiwe na maradhi ya muda mrefu kama shinikizo la damu au kisukari.

Dk. Mathias aliainisha faida za mtu akichangia damu kuwa ni pamoja na upendo na kuokoa maisha na chupa moja ya damu inaweza kuokoa maisha ya wagonjwa watatu.

Alieleza faida nyingine kuwa ni inamwezesha kupima afya bila malipo yoyote ikiwamo kujua kundi la damu, wingi wa damu shinikizo la damu, kaswende na homa ya ini.

"Uchangiaji wa damu unapunguza madini ya chuma mwilini ambapo yakizidi yanaweza kusababisha mapigo ya moyo kuongezeka, kujisikia kuchoka na kuzuia uwezekano wa kupata magonjwa ya moyo na ini," alisema.

Nao baadhi ya wachangia damu walisema kuwa uchangiaji ni jambo la upendo na wamewaomba vijana kuwa na utaratibu wa kujitolea damu mara kwa mara.

Mmoja wao, Dotto Shilogile, alisema amekuwa akichangia damu mara kwa mara na hakuna madhara yoyote anayopata.

"Niiombe jamii kujiwekea utaratibu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wagonjwa hospitalini ni ukweli usiopingika chupa moja ya damu uliochangia inaweza kuokoa maisha ya watu wasiopungua watatu," alisema Shilogile.

# Bashe aagiza ma-RC kusaka matapeli kilimo mtandaoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KUTOKANA na kuibuka kwa matapeli wanaoendesha shughuli za kilimo katika mitandao ya kijamii, Waziri wa Kilimo Husein Bashe, amewaagiza wakuu wa mikoa kufanya msako ili kuwakamata watu wanaofanya utapeli huo.

Pia, Waziri Bashe amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya waliowapa maofisa ugani kazi ya utendaji wa mitaa kuacha mara moja na badala yake wawarejeshe katika majukumu yao.

Alibainisha hayo jana katika mkutano wa 12 wa wadau wa kahawa uliofanyika jijini Dodoma kwa kushirikisha wakulima, wakuu wa mikoa na wilaya zinazolima zao la kahawa nchini.

Alisema wizara imeanza kufuatilia matapeli hao na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao ili kukomesha suala hilo huku akisisitiza kuna kesi nyingi za aina hiyo zinafika wizarani na wanaoibiwa wengi ni wastaafu, watumishi wa umma na sekta binafsi.

Alisema kumeibuka tabia ya watu kujitangaza mitandaoni kuwa wanaendesha kilimo na kuwataka watu watoe fedha ili wakawalimie mashamba, wizara haiwatambui watu hao na imeahidi kuwachukulia hatua kali kwa watakaobainika.

"Kuna kesi ipo wizarani tunasumbuka nayo mtu katapeliwa na wanaojifanya wanaendesha kilimo mitandaoni serikali hatuwezi kuruhusu utapeli kwenye sekta ya kilimo jamii inapaswa kuwa makini," alisema Bashe.

Wizara pia imetoa wito kwa kila mwenye nia ya kutaka kulima aende wizarani au kwenye halmashauri achukue ardhi kwa ajili ya kilimo na sio mitandaoni.

Alifafanua kuwa hakuna kilimo cha kwenye mitandao kama watu wanataka kuwekeza ni lazima waende shambani na sio kurubuniwa na watu wa mitandaoni ambao huenda kuwaonyesha mashamba ya kitapeli yakiwa yamebandikwa jina la muhusika aliyelipa pesa akiondoka wanatoa kibao.

Akizungumzia kuhusu maofisa ugani wanaofanya kazi za utendaji, aliwataka wakuu wa mikoa kuwarejesha katika majukumu yao maofisa kilimo.

Aidha, aliwaagiza kuwasilisha vipimo vyao wizarani kwa ajili ya kushonewa sare kama walivyopangiwa na akisisitiza kuanzia mwakani watakuwa wakitumiwa fedha kwa ajili ya kununua sare za utendaji ambazo zitawatambulisha kwa wakulima.

Alisema pia wanatarajia kuwakabidhi magari maafisa kilimo kila wilaya ili kurahisha utendaji kazi wao wa kuwafikia wakulima katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo, alisema wizara imejipanga kuwatumia Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Wananchi (JWTZ) kwa ajili ya kuwafundisha maofisa ugani ili kuweka nidhamu kwenye kilimo.





# Wahudumu afya watakiwa kuzingatia matumizi dawa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MENEJA wa Mamlaka ya Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi (TMDA) mikoa ya nyanda za juu kusini, Anitha Mshighati, amewakumbusha wahudumu wa vituo vya afya na zahanati, kuzingatia matumizi ya dawa na vifaa tiba kwa kuhakikisha hawatumii dawa zilizokwisha muda wake ili kutohatarisha afya za wananchi.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe juu ya uelewa wa watoa huduma za afya katika matumizi ya dawa zilizokwisha muda wake.

Hivyo, aliwakumbusha wahudumu na wataalamu wa afya kuzingatia matumizi ya dawa na vifaa tiba katika maeneo yao, kwa kuhakikisha wanazingatia ubora na ukomo wa matumizi kabla ya kuwapatia wagonjwa wanaofika kwa ajili ya kupata matibabu.

"Katika ukaguzi wetu hadi sasa tumebaini asilimia 46 ya dawa zilizopigwa marufuku katika maeneo mbalimbali ikiwamo maduka na vituo vya afya vilevile tulibaini asilimia 19 ya dawa zinazouzwa zimekwisha muda wake, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi na wataalamu wa afya kuzingatia ubora na ukomo wa dawa ili kulinda afya za watumiaji," alisema Mshighati.

Alieleza kuwa bado wanaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara pamoja na doria kwenye mipaka na maeneo yanayohisiwa kutumika kuingia magendo na kutoa tahadhari kwamba wanaobainika wanaendelea kuchukuliwa hatua ikiwamo kufikishwa mahakamani na kutaifishwa bidhaa zao.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, aliwaomba wataalamu pamoja na wahudumu wa afya kushirikiana na TMDA kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na matumizi ya dawa zinazohitajika ili kulinda afya za wananchi.

Alisema ni muhimu kwa wataalamu na watoa huduma za afya kuzikagua dawa ili kujua muda wa matumizi kabla ya kuwapatia wagonjwa na kwamba kwa kufanya hivyo kuepusha na madhara yatokanayo na matumizi ya dawa zilizokwisha muda wake.



Mdau wa Maendeleo Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, akiwashukuru viongozi wa mila wa kabila la Wasafwa kwa kufanya uamuzi wa kwenda kujenga nyumba ya kabila hilo katika Kijiji cha Makumbusho mkoani Dar es Salaam, pia aliwachangia Sh. 400,000 kwa ajili ya kufanikisha mradi huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maduka pembejeo yafunguliwa kuwasaidia wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MADUKA 28 ya pembejeo za kilimo yameanzishwa mikoa ya Nyanda ya Nyanda za Juu Kusini lengo likiwa kuwasaidia wakulima kupata mbegu na mbolea bora kwa wakati.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya Ekari Moja Tanzania, Dorcas Tinga, wakati wa uzinduzi wa maduka 12 kati ya 28 ambayo yamezinduliwa mkoani Mbeya.

Alifafanua kuwa maduka 16 yalifunguliwa mkoani Njombe, maduka tisa yapo Mbeya na matatu yapo Songwe na kwamba yote yanakidhi vigezo vya utoaji huduma bora za pembejeo za kilimo.

"Katika kuhakikisha kampuni yetu inamjali mkulima tulianzisha programu ya kuwakopesha wakulima pembejeo za kilimo pamoja na mafunzo ili wazalishe kwa tija na kwamba hadi sasa wakulima 60,000 wa mikoa ya Nyanda za Juu kusini wamenufaika," alisema Tinga.

Miongoni mwa wakulima wanaonufaika na kampuni hiyo, Teresia Mponzi kutoka Imezu alisema elimu ya kilimo bora imekuwa msaada kwao kwa sababu wanalima kwa tija na kujiongezea kipato.

Aliiomba Kampuni ya Ekari Moja Tanzania kuendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu na elimu ili wakulima wanufaike na kujikwamua kiuchumi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua aliipongeza Kampuni ya Ekari Moja Tanzania, kuwekeza katika tafiti na teknolojia ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa wakulima ambapo walianza na vijiji vitatu vyenye wakulima 433 mwaka 2016.

Alifafanua hadi sasa wakulima 6,957 wa vijiji 37 kwenye msimu wa kilimo 2021/2022 wamenufaika na kwamba wakulima wanaendelea kupata tija na manufaa kutoka kampuni hiyo.

# Washauri vijana kuchangamkia fursa kiuchumi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

VIJANA mkoani Mbeya, wameshauriwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza kupitia mashirika na taasisi ili kujikwamua kiuchumi.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Mkurugenzi wa Rafael Group linalojihusisha na uuzaji na usambazaji wa nafaka mbalimbali jijini Mbeya, Rafael Ndelwa.

Alisema ili vijana waweze kutimiza malengo yao lazima kuheshimu ndoto za maisha yao badala ya kushiwishika na wenzao na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa.

Alisema kwa sasa kampuni yake ina uwezo wa kukuposha pembejeo za kilimo wakulima wa mazao kama vile maharage mpunga, ngano, kwamba baada ya mavuno wakulima hao humpatia mavuno kulingana na gharama za pembejeo zilizotolewa.

Alisema zaidi ya wakulima 100 wamenufaika na fursa hiyo na kumwezesha yeye kuwa na akiba ya mazao mengi ambayo na yeye huyachakata kisha kuuza ndani na nje ya nchi.

Alisema ameweza kuweka mashine kubwa za kisasa kwa ajili ya kusaga nafaka kama vile mpunga katika kampuni yake na kuyapaki kwenye vifungashio vyenye nembo ya kampuni yake.

Hivyo, aliwashauri vijana kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri kwa kuhakikisha wanajiunga kwenye vikundi ili waweze kukopesheka na kuanzisha shughuli za kujikwamua na umaskini.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Suma Fyandomo, alisema katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanafanya shughuli zao wakiwa na afya alitoa Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuwakatia bima wananchi 500.

Alieleza sababu ya kufanya hivyo ni kuhakikisha wananchi wanapata matibabu bila kikwazo chochote ili kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali bila tatizo.





Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama (kulia), akipokea zawadi kwa Kamishna wa Bima Tanzania (TIRA), Baghayo Saqware, baada ya kufunga mafunzo kwa watumishi wa TIZA kuhusu bima mtawanyo yaliofanyika Mjini Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaeleza umuhimu bima mtawanyo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema bima mtawanyo ni muhimu katika kuhakikisha biashara ya bima nchini inakuwa himilivu na kusaidia upatikanaji wa mitaji mikubwa kutoka katika mataifa ya nje. Aliyasema hayo mjini hapo wakati akifunga mafunzo kwa watendaji wa Mamlaka ya Bima Tanzania (TIZA) kuhusu bima mtawanyo ili kufidia majanga yanapotokea.

Alisema wananchi wengi wanapata matatizo mbalimbali ikiwamo majanga kwenye kilimo, mazao kuharibiwa na hali ya hewa, lakini hawajui kuwa kuna bima ya kilimo. Alisema ajali mbalimbali zinazotokea zinaacha majonzi makubwa na athari kubwa inakwenda katika uchumi na alitaka TIZA kusimamia kuhakikisha soko la bima linakuwa na uwezo wa kuwa ni suluhisho na kinga kwa kila jambo. Alisema kumejitokeza matukio mengi ya masoko kuungua moto, lakini jambo la kushangaza masoko hayo hayakuwa na bima na wananchi pia hawana utamaduni wa kukata bima vitu vyao vya thamani ikiwamo nyumba. Alitaka mamlaka hiyo kutoa elimu ya umuhimu wa kutumia bila ya kujikinga na majanga.

"Bima ni uchumi wa taifa hivi asilimia 99 wakijua kuna bima na kuchukua hatua mtakuwa mmeweka mtaji wa kiasi gani katika benki zetu kwa ajili ya kukuza uchumi wetu, lakini mtakuwa mmeokoa Watanzania wengi watakaokuwa wameingia katika majanga mbalimbali katika shughuli na maisha ya kila siku," alisema.

Alisema tangu Rais Samia Suluhu Hassan, ameongoza nchi, amefanya mageuzi makubwa katika kila sekta, ameipongeza TIRA kwa maamuzi hayo sahihi ya utoaji wa mafunzo hayo kwa watendaji wake.

Aliipongeza TIZA kwa kuvutia wawekezaji wengine kwa kuzindua mwongozo wa bima ya kiislamu (Takaf) na kwamba mfumo wa bima hautakuwa kandamizi.

Akizungumzia bima mtawanyo, alisema watakapokuwa wabobezi katika bima hiyo na kutoa uwezo wa kitaaluma kwa watendaji wa mamlaka kusimamia anuai zote zinazohusiana na majanga, itakuwa wamemsaidia Rais Samia kufungua uwekezaji nchini.

"Tuna jukumu la kuongeza nguvu na spidi katika maono, matashi na matamanio ya serikali kuhakikisha tunavutia mitaji mingi ya kutosha, sisi tujione ni sehemu ya kusaidia hiyo mitaji kuingia katika taifa letu," alisema.

Pia, alisema rasilimali watu zikifanya kazi vizuri hata rasilimali zingine zitafanya vizuri katika ujenzi wa taifa ili kujenga mifumo ya kidigitali na kuwakumbusha kuwa taifa linawategemea.

"Niwapongeze mamlaka kwa gawio la serikali kwa mwaka 2022 mmechangia Sh. bilioni 2.4... gawio hili sihaba tukijipanga tukafanikiwa zaidi mwakani linaweze kupata zaidi ya hizi ambapo gawio hilo linasaidia katika huduma mbalimbali ikiwamo elimu na afya," alisema. Naye Kamishna wa Bima, Baghayo Saqware, alisema matarajio yao ni kwamba watumishi hao wa mamlaka watachambua na kusaidia upatikanaji wa huduma za bima mtawanyo.

Alisema changamoto iliyoko wanahitaji kuwa na kampuni za bima mtawanyo nyingi hivyo wamewaelekeza watumishi wao kutengeneza utaratibu wa kuwezesha kutoa fursa za kusajili kampuni za bima na kuwashauri wawekezaji wa ndnai na nje ya nchi kuwekeza Tanzania.

"Masharti yetu yanafanana na nchi zote za Afrika Mashariki kinachohitajika ni kuwa na wawakilishi ambao watafanya kazi kwa uweledi," alisema. Kwa upande wao watendaji waliopatiwa mafunzo hayo walisema wamejifunza vitu vingi ikiwamo kutetea uchumi wa taifa kwa kuhakikisha fedha ambazo zilitakiwa kwenda nje kukidhi majanga makubwa kampuni za bima kutunza kiwango cha fedha hicho.

# Vyuo vikuu vyatakiwa kuanzisha mitaala ya kujiajiri

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Abdul Gulan, amevitaka vyuo vikuu kuanzisha mitalaa itakayowandaa wanafunzi kujiajiri badala ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema wimbi kubwa la vijana wanapomaliza masomo ya elimu ya juu husubiri kuajiriwa hasa serikali wakati ajira zinazotolewa ni chache na kwamba ni vyema vyuo vikuu kuwandaa wanafunzi kujiajiri.

Kauli hiyo aliitoa, wakati akifungua maonyesho ya tatu ya elimu ya juu yaliyofanyika viwanja vya Mapinduzi Square mjini Zanzibar.

Akizungumzia lengo la maonesho hayo alisema ni kuwajengea uwezo wanafunzi katika kutambua masomo ya kujiunga nayo kulingana na viwango vyao vya elimu hivyo ni vyema wazazi na wanafunzi wayatumie katika kufikia lengo hilo.

Aliwapongeza mawakala wa vyuo kwa kusimamia shughuli za kuwapeleka wanafunzi katika vyuo vya nje ya nchi kwa lengo la kuongeza taaluma hasa za teknolojia kwa faida ya taifa.

Aliwaomba wazazi na walezi kujitahidi kuwahimiza watoto kusoma kwa bidii na kuitumia fursa ya maonyesho hao ili waweze kujipatia ujuzi kwa kuwa taifa linahitaji vijana ambao watasaidia katika nyanja mbalimbali na kukuza maendeleo ya elimu nchini kwao.

Aliziomba taasisi na vyuo vikuu kushirikiana pamoja na wizara ili kufikia lengo la kuhakikisha elimu inayotolewa inaleta manufaa kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Naye Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Ali Khamis, alisema lengo lao ni kuhakikisha juma la elimu ya juu linafanyika kila mwaka ili kukusanya vyuo vikuu vilivyokuwapo na kutumia fursa mbalimbali zilizokuwapo nchini.

Alisema maendeleo ya nchi hayaletwi na mtu pekee bali ni lazima kushirikiana na mawakala wa vyuo vikuu na serikali zimetambua kuweka taratibu na sheria kwa watu hao na wamekuwa ni sehemu na chachu kubwa ya kuanzisha maonyesho hayo toka yalipoanzishwa.

Kwa upande wake Meneja Masoko wa wakala wa elimu ya juu Uturuki kutoka kampuni ya Shems Group, Zakia Mohamed Juma, alisema wanapofanya usahili wa wanafunzi wanaangalia zaidi uelewa wa mwanafunzi kulingana na mahitaji ya taifa.

"Kinacholengwa ni mwanafunzi anaelewa nini na zaidi akienda kusoma huko nje ataleta ujuzi gani kuisaidia nchi yake maana tunajua Uturuki ni nchi ambayo imepiga hatua kwa hiyo mwanafunzi akitoka kule aje na ujuzi tofauti na sio kwenda kutembea," alisema Zakia.

Mkuu wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, alisema mpaka sasa kuna mawakala 23 waliosajiliwa nchini kwa ajili ya kuwapeleka wanafunzi kusoma nje ya nchi na kuwataka wazazi na wanafunzi kuwatumia mawakala hao wanaotambuliwa kisheria.

Alisema umuhimu wa kutumia mawakala wanaotambuliwa ni kudhibiti ubora wa elimu kuepuka kwenda kusoma katika vyuo ambavyo havitambuliki na mataifa yao na kujikuta wanatapeliwa.

Maonyesho hayo ni ya tatu kisiwani hapo tangu yalipoanzishwa mwaka 2019 na jumla ya washiriki mwaka huu ni 32 ikilinganishwa na 22 wa mwaka jana.

# 'Wazazi wa kiume msikimbie majukumu ya malezi'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Ustawi wa Wilaya ya Kati Unguja, Ali Shehe Kombo, amewataka wazazi wa kiume kuacha kukimbia majukumu yao ikiwamo malezi kwa familia zao na matunzo kwa watoto.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wanajamii na wanafunzi wa madarasa mbalimbali za Wilaya ya Kati, ikiwa ni maadhimisho ya mtoto wa Afrika.

Alisema licha ya matukio ya udhalilishaji ikiwamo ubakaji na ulawiti kuripotiwa katika vyombo vya sheria, pia kuna wimbi kubwa la utelekezaji wa watoto.

Alisema utelekezaji huo unatokana na wanaume kukimbia majukumu yao na kuwaachia mzigo mkubwa wa malezi wanawake peke yao jambo ambalo linachangia watoto kudhalilishwa.

Alisema utelekezaji huo unajitokeza ndoa inapovunjika, wanawake na watoto kuwa waathirika zaidi wa vitendo vya udhalilishaji.

Alisema watoto wanastahiki kulelewa na kupatiwa huduma zote ili kuimarisha maisha yake ya sasa na baadaye.

Aliitaka jamii kuwa karibu na watoto wao ili kuwabaini na matendo ya udhalilishaji wanayofanyiwa kabla ya kupata athari kubwa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwajua watoto mapema wanapofanyiwa vitendo hivyo na kuchukua hatua za haraka.

Ukaribu na mtoto, alisema ni njia sahihi ya kumfanya kutokuwa na hofu ya kueleza madhila wanayofanyiwa.

"Asilimia kubwa ya watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo huchelewa kujulikana kutokana na wazazi na walezi kutokuwa karibu na watoto wao kutokana na kuwa na hofu na hata wakijulikana huwa tayari wameshaathirika sana," alisema.

Akiwasilisha mada ya udhalilishaji dhidi ya watoto, Ofisa kutoka Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzanzia (TAMWA), Zanzibar, Saphia Ngalapi, aliwasisitiza vijana wanapofanyiwa vitendo hivyo wasikae kimya kutokana na vitendo hivyo vinaumiza kisaikolojia na kuvuruga mfumo mzima wa maisha yao.

Sheha wa Shehiya ya Machui, Abdalla Salum Juma, alifurahi kutolewa elimu hiyo ndani ya shehia yake na alisisitiza asasi hizo kuandaa elimu hiyo ili jamii ipate uelewa wa kujikinga na vitendo hivyo.

Safia Leghela, Mratibu wa Jukwaa la Jumuiya ya Haki za Watoto Zanzibar ZCRF, alisema ili kuwalinda watoto na vitendo hivyo ni lazima wenyewe wajue kujilinda.

# TIOB, TAMFI kuimarisha huduma ndogo za kibenki

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI ya Taaluma za kibenki (TIOB) na Muungano wa Taasisi zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha Tanzania (TAMFI), wameingia makubaliano ya ushirikiano wa kutoa mafunzo ya weledi, misingi na miongozo kwa taasisi zinazotoa huduma ndogo za kibenki nchini.

Akizungumza baada ya kusaini makubaliano hayo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TIOB, Patrick Mususa, alisema mafunzo hayo yanalenga kuboresha sekta ya utoaji huduma ndogo za kibenki kwa kuwajengea uwezo watoa huduma hizo.

"Tunataka kuinua maeneo madogo ya kiuchumi ili kukuza sekta hii kupitia kujenga weledi kwa watoa huduma ili kuwapa uwezo watendaji na wanufaika wa huduma hizi," alisema.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa TAMFI, Winnie Terry, alisema jitihada za kuwa na ushirikiano huo zilianza muda mrefu na lengo la ushirikiano huo ni kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wadau wa sekta hiyo nchini.

"Katika makubaliano haya tutashirikiana kutoa semina, kongamano, utafiti na ushauri wa kibiashara na uandaaji majarida katika sekta hii kwa wanachama wetu ili kutoa huduma bora katika biashara hiyo na kuimarisha sekta hii," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa hapo mwanzo walikuwa wakishirikiana kutoa huduma hiyo na taasisi zilizopo nje ya nchi, lakini safari hii wakaona umuhimu wa kushirikiana za taasisi ya ndani ili kuwa na uelewa zaidi na mwenendo wa utoaji huduma hizo nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), Tusekele Joune, alisema kuwa amefurahi kuwa taasisi hizo mbili zimeungana kutoa mafunzo hayo kwa kuwa zitazalisha watoa huduma wenye weledi na kuboresha huduma hiyo nchini.

"Ninafurahi kuwa mmoja wa mashuhuda wa tukio hili muhimu na ninaunga mkono kwa kuwa tunajua mwisho wa siku watakaozalishwa katika mafunzo hayo ndiyo tutakaowachukua sisi ili watufanyie kazi, kwa hiyo hongereni sana," alisema.

# SBL yatumia bil.1.5/- kusambaza maji

**Na Frank Monyo**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imesema imetumia zaidi ya Shilingi bilioni 1.5 katika kufadhili miradi ya maji sehemu mbalimbali hapa nchini.

Mkurugenzi wa Uhusiano kwa Umma wa SBL, John Wanyancha, aliyasema hayo na kueleza kuwa wametumia kiasi hicho cha fedha katika kipindi cha miaka 10, kwamba wamechimba visima 20 sehemu mbalimbali hapa nchini.

Wanyancha alisema kampuni hiyo inachukulia maji kama moja ya mahitaji muhimu kwa maendeleo ya watu na ndiyo sababu imekuwa mstari wa mbele kushirikiana na serikali pamoja na wadau wengine kusaidia upatikanaji wa majisafi na salama kwa Watanzania.

Alisema SBL imesaidia upatikanaji wa maji na salama kwa watu milioni mbili na kuongeza kuwa miradi hiyo imelenga zaidi jamii ambazo zinauhitaji mkubwa wa huduma hiyo.

"Pamoja na kusaidia jamii zenye shida ya maji moja kwa moja, miradi yetu pia imekuwa ikizisaidia taasisi mbalimbali za kijamii na mfano mzuri ni Mradi wa Karatu ambao umepanuliwa na kuweza kutoa huduma kwa shule nne na kituo cha afya wakati mradi wa Pasua Moshi umeweza kusaidia upatikanaji wa maji kwa shule tatu na soko lililoko jirani," alisema Wanyancha.

Aliongeza: "Miradi yetu huwa jirani na maeneo ambayo SBL hununua nafaka kwa ajili ya utengenezaji wa bia. Husaidia kuwapatia wakulima zaidi ya 400 maji kwa ajili ya umwagiliaji."

Alisema miradi ya maji ya SBL imekuwa ikisaidia na kuunga mkono jitihada za serikali kuwapatia wananchi huduma ya majisafi na salama katika maeneo ambayo yanashida.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, alipokuwa akielezea maoni ya taasisi hiyo kuhusu bajeti ya 2022/223 na kushauri serikali kuondolea kodi inayopangwa kutozwa kwa watu wa kuanzia miaka 18. Kulia ni katibu mkuu wa taasisi hiyo, Hamad Tao na mjumbe wa kamati ya utendaji ya CEGODETA, Zakiah Ramadhan. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TCDC yavitaka vyama ushirika kuweka juhudi

**Na Gwamaka Alipipi**

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imevitaka vyama vya ushirika nchini kuweka juhudi ili kufanikisha sekta ya kilimo inapiga hatua.

Rai hiyo imetolewa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara, Dk. Benson Ndiege, akieleza kuwa serikali imetenga bajeti kubwa kwenye kilimo kwa mwaka wa ujao.

Alisema bajeti hiyo inatarajiwa kwenda kuimarisha katika ujenzi wa miundombinu ya kilimo kama vile umwagiliaji, uzalishaji, utumiaji wa mbegu bora na mbolea.

Dk. Ndiege alisema ili kufikia lengo la bajeti, vyama vya ushirika ni lazima vitekeleze jukumu lao la msingi la kuratibu na kuwasimamia wakulima.

Akielezea kuhusu umuhimu wa nafasi ya vyama vya ushirika, Dk. Ndiege alisema, kwa kuwa bajeti ya kilimo imejielekeza katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, vyama vya ushirika vitakuwa ni chombo muhimu katika kusimamia na kuratibu wakulima, ili wamwagilie kwa utaratibu mzuri.

"Ili miundombinu hiyo iwe endelevu, ni lazima uwasimamie wakulima. Ni lazima uwe na mfumo wa kuwasimamia ili watumie miundombinu hiyo vizuri," alisema Dk. Ndiege.

Kadhalika, alisema bajeti ya mwaka ujao inatarajiwa kuongeza uzalishaji katika kilimo, hali ambayo itahitaji masoko zaidi, vyama vya ushirika vitahitajika kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika.

Alisema wiki iliyopita TCDC ilisaini mkataba na Benki ya NMB wa Sh. bilioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya mazao kwa vyama vya ushirika nchini.

Alisema ujenzi wa maghala hayo utasaidia kuongeza uhifadhi na masoko kwa wakulima.

"Kwa vile inategemewa kuwa bajeti itaongeza uzalishaji katika kilimo, makubaliano hayo yanatarajiwa kuokoa mazao yanayopotea kutokana na kukosekana kwa miundombinu ya kuhifadhi," alisema Dk. Ndiege.

Dk. Ndiege alisema kutokana na matatizo ya kukosekana kwa maghala, serikali kupitia Tume ya Ushirika iliona ni muhimu kukaa na NMB na kujadili namna ya kutatua matatizo hayo.

HABARI KIMATAIFA

# Ecuador yatangaza dharura kukabili wimbi maandamano

**QUITO, Ecuador**

RAIS wa Ecuador, Guillermo Lasso, ametangaza hali ya dharura kwenye majimbo matatu ya nchi hiyo kujaribu kutuliza maandamano ya jamii za wazawa wanaotaka kupunguzwa kwa bei ya mafuta.

Akilihutubia taifa kwa njia ya televisheni kiongozi huyo alisema uamuzi huo wa kuyaweka chini ya hali ya dharura majimbo matatu ikiwamo mji mkuu Quito ni sehemu ya dhamira yake ya kuilinda nchi hiyo na kuimarisha utii wa sheria.

Amri hiyo inamwezesha rais kutuma vikosi vya jeshi kwenye majimbo hayo kurejesha utulivu, kusitisha haki za kiraia na kutangaza marufuku ya kutoka nje.

Kwa siku ya sita mfululizo makundi ya wenyeji wa asili katika taifa hilo lenye utajiri wa mafuta yanafanya maandamano ya nchi nzima kupinga hali ngumu ya maisha ikiwamo kupanda kwa gharama za nishati hiyo.

**DW**

# Mwanamfalme kuzuru Misri, Jordan na Uturuki

**RIADH, Saudia Arabia**

MRITHI wa kiti cha ufalme wa Saudi Arabia, mwanamfalme Mohammed bin Salman, leo anatarajia kuanza ziara ya kikanda katika nchi za Misri, Jordan na Uturuki.

Taarifa iliyotolewa na ufalme huo, ilisema ziara hiyo ya mwanamfalme bin Salman kuwa atajadiliana na viongozi wa mataifa hayo masuala ya kikanda, kimataifa na ushirikiano wa siku za usoni.

Kituo cha kwanza cha ziara hiyo kitakuwa Misri na kisha ataelekea Jordan na baadaye ataitembelea Uturuki. Inatarajiwa kutakuwa na kuwekeana saini kwa mikataba ya uwekezaji na nishati.

Ziara yake nchini Uturuki ndiyo itafuatiliwa kwa karibu kutokana na kulegalega kwa mahusiano kati ya Saudi Arabia na nchi hiyo tangu mkasa wa kuuliwa kwa mwandishi habari wa kisaudi Jamil Khashoggi mjini Instabul mwaka 2018.

**DW**

# Zelensky atembelea uwanja wa vita kusini mwa Ukraine

**KYIV, Ukraine**

RAIS wa Ukaine, Volodymyr Zelensky, ametembelea kwa mara ya kwanza eneo lililoharibiwa kwa vita kusini mwa nchi hiyo kujionea madhara na kuwashukuru wanajeshi wa nchi yake walio mstari wa mbele.

Katika ziara hiyo ya nadra kufanywa na kiongozi huyo nje ya mji mkuu Kyiv, Zelensky aliuzuru mji wa Mykolaiv ulio kwenye mwambao wa bahari nyeusi na kisha kuwatembelea wanajeshi karibu na eneo hilo na kwenye mkoa jirani wa Odessa.

Mji wa Mykolaiv ni miongoni mwa maeneo ya kimkakati yanayolengwa na Russia kwa kuwa unapatikana kwenye njia ya kuelekea bandari muhimu ya Odessa kwenye bahari nyeusi.

Katika wiki za hivi karibuni vikosi vya Russia vimewekeza nguvu kuyadhibiti maeneo ya kusini na mashariki mwa Ukraine ikiwamo eneo la bahari nyeusi.

**NATO YAONYA VITA KUCHUKUA MIAKA MINGI**

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami ya NATO, Jens Stoltenberg, ameonya kuwa vita ya Russia na Ukraine inaweza kuendelea kwa miaka mingi na mataifa ya magharibi hayapaswi kurudi nyuma katika kuisaidia nchi hiyo.

Akizungumza kwenye mahojiano na gazeti la Bild am Sonntag la nchini Ujerumani, Stoltenberg alisema nchi za Jumuiya ya NATO ni lazima zijitayarishe na ukweli huo kuwa vita nchini Ukraine inaweza kudumu kwa muda mrefu na ni muhimu kuendelea kuipatia msaada.

Aliongeza kwamba kuipatia Ukraine msaada wa silaha za kisasa kutatanua nafasi ya vikosi vya nchi hiyo kulikomboa jimbo la mashariki la Donbas ambalo limeangukia mikononi mwa Russia.

Kiongozi huyo pia alisema mkutano wa wakuu wa nchi wa Jumuiya ya NATO utakaofanyika mjini Madrid nchini Uspania baadaye mwezi huu, unatarajiwa kufikia makubaliano ya kuisaidia Ukraine kuboresha zana zake za vita na kuachana na zile za enzi ya dola ya kisovieti.


**SCHOLZ ASEMA G7 LITAENDELEA KUISAIDIA**

Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz, amesema kundi la mataifa yaliyostawi kiuchumi duniani la G7, litautumia mkutano ujao wa wakuu wa nchi kuweka wazi azma yake ya kuendelea kuisaidia Ukraine kwa kipindi kirefu kadri itakavyohitajika.

Kwenye mahojiano na shirika la habari la Ujerumani, kansela Scholz, alisema anataka kuutumia mkutano wa kilele wa G7 utakaofanyika wiki ijayo katika jimbo la Bavaria kujadili matarajio ya muda mrefu kwa Ukraine. Alikaririwa akisema mataifa ya kundi hilo yataendelea kuisaidia nchi hiyo kwa kipindi kirefu na yanalenga kuhakikisha Russia haipati mafanikio iliyokusudia wakati ilipoamua kuivamia kijeshi Ukraine.

Scholz ambaye aliitembelea Ukraine mapema wiki hii pamoja na viongozi wa Ufaransa, Italia na Romania alisema walijadiliana na Rais Volodymyr Zelensky, kuhusu msaada ziada wa silaha hususani makombora na mizinga.

***DW***



Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy, akiwa na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz na Rais wa Romania, Klaus Lohannis, viongozi hao walipomtembelea mjini Kyiv kuonyesha uungaji mkono hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Rwanda yadai waasi wa FNL waua wawili

**KIGALI, Rwanda**

POLISI nchini Rwanda wamesema watu walioitwa kama majambazi wenye silaha wanaoshukiwa kuwa waasi wa National Libération Front (FLN) wamewapiga risasi na kuwaua watu wawili na kuwajeruhi wengine sita.

Tukio hilo limetokea jana katka majira ya saa nane mchana eneo la Kitabi kwenye barabara ya Nyamagabe na Rusizi ambayo inapitia msitu wa Nyungwe kusini magharibi mwa nchi hiyo.

Waliojeruhiwa walihamishwa hadi hospitali ya Kigeme na hospitali ya mafunzo ya chuo kikuu huko Butare.

Polisi walisema washambuliaji hao walitokea upande wa pili wa mpaka.

Msitu wa Nyungwe ni mojawapo ya maeneo ya mpakani na Burundi.

Hapo awali, nchi hizo mbili za Afrika Mashariki zilibadilishana tuhuma za kuwaunga mkono waasi wanaotaka kupindua serikali.

Kundi la waasi la FLN bado halijatoa maoni yoyote.

Kundi hilo lilianza mashambulizi dhidi ya Rwanda ikiwa linadai nyadhifa za jeshi.

Taarifa ya polisi inasema iliingilia kati kwa dakika chache katika tukio hilo.

Ilieleza taarifa hiyo kuwa washambuliaji wanafuatiliwa," inaongeza.

***BBC***

## HABARI MICHEZO

# YANGA YATAMBA ITAMALIZA MSIMU KWA KUTOA VICHAPO

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kwamba tayari wametwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, Klabu ya Yanga imesema haitakuwa na huruma yoyote katika kuhakikisha inashinda michezo yake mitatu ya ligi hiyo iliyosalia msimu huu.

Yanga imebeba ubingwa wa ligi hiyo ikiwa na mechi tatu mkononi kabla ya msimu huu wa 2021/22 kumalizika rasmi Juni 29, mwaka huu.

Mkurugenzi wa Mashindano wa klabu hiyo, Thabit Kandoro, amesema kuelekea mchezo wao ujao dhidi ya Polisi Tanzania na mingine miwili iliyobaki hawatakuwa na huruma na timu yoyote.

Akizungumza jijini jana, Kandoro alisema si jambo rahisi kukaa miaka minne bila ubingwa, hivyo lazima washinde michezo yao hiyo ili kumaliza msimu vizuri na kwamba mechi ya keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Polisi Tanzania, kamwe hawatalegeza kamba.

"Timu ipo vizuri kutoa burudani kwa mashabiki wao na kila mchezaji anataka ushindi kwenye michezo yote iliyobakia," alisema Kandoro.

Alisema huo ni mchezo wa mwisho kwao msimu huu kucheza jijini Dar es Salaam, hivyo anawaomba mashabiki pamoja na wadau mbalimbali wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi.

Kondoro alisema baada ya mchezo huo wataelekea mkoani Mbeya kuvaana na Mbeya City Juni 25 na baada ya hapo watakwenda mkoani Arusha kwa ajili ya mchezo wao wa mwisho msimu huu dhidi ya timu ya Mtibwa Sugar.

"Tunashukuru mchezo wetu wa mwisho tutaucheza na timu ya Mtibwa Sugar mkoani Arusha ambapo tutakuwa tunawasubiri Coastal Union kupambana nao kwenye Fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC)," alisema.

## Malwisi ageukia vipaji vya soka

**Na Cheji Bakari, Tanga**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Mbeya Kwanza FC ya jijini Mbeya, Maka Malwisi, amesema baada ya kuachana na klabu hiyo, hana mpango wa kutafuta timu ya kufundisha badala yake ameamua kujikita katika Kituo cha Foysa Academy kuendeleza vipaji vya michezo.

Akuzungumza kwa njia ya simu na mwandishi wa habari hizi, Malwisi amesema kwa sasa yupo mkoani Mtwara ambapo ameanzisha kituo chake binafsi cha kuendeleza vipaji vya soka.

"Kwa sasa sina mpango wa kutafuta timu, nimeamua nishughulike na Academy yangu ambayo ipo hapa mkoani Mtwara inaitwa Forest Youth Soccer Aspirant (Foysa)," alisema.

Aliongeza: "Kwasasa ni kituo kutokana hatuna madarasa ila ndio tumepata kiwanja, lakini baadaye tukishapata madarasa tutajenga shule."

Malwisi ambaye nafasi yake Mbeya Kwanza FC imechukuliwa na Kocha Mbwana Makata, ambaye naye alitupiwa virago kutoka Dodoma Jiji FC baada ya raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara kumalizika na timu hiyo kuwa na mwenendo mbaya, akitoa maoni yake kuhusu timu hiyo kufanya vibaya alisema kwa sasa uongozi wa klabu hiyo lazima ukubaliane na hali halisi.

"Kwa sasa timu ilipofika lazima wakubaliane na hali halisi, warudi wakajipange upya," alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara Mbeya Kwanza FC inaburuza mkia ikiwa na pointi 24 baada ya michezo 27.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul (wapili kushoto), akishiriki mazoezi ya mchezo wa Yoga yaliyofanyika katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni siku rasmi ya kuadhimisha mchezo huo duniani. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

# Gekul: Mazoezi ya Yoga yapewa kipaumbele

**Na Faustine Feliciane**

NAIBU Waziri wa Utamaduni Sanaa na Michezo, Pauline Gekul, amewataka Watanzania kushiriki mazoezi ya mchezo wa Yoga ili kuimarisha afya ya kimwili na kiroho.

Akizungumza jana katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kwenye maadhimisho ya Siku ya Mchezo wa Yoga duniani, ulioasisiwa nchini India, Gekul alisema mchezo huo umekuwa maarufu ulimwenguni kote kutokana na faida yake, hivyo Watanzania washiriki kuimarisha afya zao.

"Niupongeze Ubalozi wa India hapa nchini kwa jitihada zao za kuutangaza na kuufundisha mchezo huu hapa Tanzania, kwetu sisi Watanzania hii iwe fursa kwetu kuendelea kuucheza mchezo huu na kuusambaza zaidi, kwa kushiriki michezo, inasaidia kupambana na magonjwa yasiyoambukiza kama kisukari na presha," alisema Gekul.

Alisema anatambua mwaka huu ni wa nane kuadhimishwa mchezo huo wa Yoga, lakini tayari umeanza kupata umaarufu mkubwa.

Aidha, alisema serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, inajali na itaendelea kujali kila kitu kinachompa Mtanzania kuishi kwa amani na afya.

"Ni vema sasa mazoezi ya Yoga yakachukuliwa kwa umuhimu wake ili wananchi waweze kujenga umoja, mshikamano na kuboresha afya ya mwili na akili," alisema Gekul.

Kwa upande wa Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan, alisema mazoezi ya Yoga ni muhimu kwa afya, hivyo Watanzania washiriki mara kwa mara.

Alisema ingawa maadhimisho hayo yanafanyika Juni 21, kwa Tanzania wameamua kuadhimisha jana, Jumapili kutokana na tarehe husika ambayo ni kesho, kuangukia siku ya kazi.

"Kwa hapa Tanzania mikoa mitano inaadhimisha siku ya mchezo huu, hii ni kuonyesha namna gani mchezo huu umekuwa na umuhimu mkubwa kwa afya ya mtu, ubalozi utaendelea kushirikiana na Watanzania katika kuimarisha mchezo huu," alisema Balozi Pradhan.

Pradhan alisema kwa nchini kwao, India siku ya maadhimisho ya mchezo huo ni mapumziko na na wananchi washiriki mchezo huo.

Kwa Dar es Salaam zaidi ya watu 3000 walishiriki mazoezi ya kuadhimisha mchezo huo yaliyofanyika Uwanja wa Uhuru.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMRUDIA HAALAND
BAADA ya kumkosa Kylian Mbappe, Real Madrid tayari inapanga kufikia kiwango cha euro milioni 150 kilichowekwa na Manchester City ili kumwachia Erling Haaland kwa kutaka kumsajili mwaka 2024. ***(AS)***

### STERLING ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA inamwania mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27. ***(Fabrizio Romano, via Express)***

### UNITED NA PUNGUZO BARCA
MANCHESTER United ina matumaini Barcelona watapunguza ada ya pauni milioni 80 waliyoiweka kwa pauni milioni 10 hadi 15 ili kumuuza kiungo wao kimataifa wa Ufaransa, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Athletic)***

### TEN HAG AMTAKA ERIKSEN
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amewaambia mabosi wa klabu hiyo kumsajili kiungo wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 30. ***(Mirror)***

### LIVER KUMPOTEZA SALAh
LIVERPOOL inajiandaa kumpoteza Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 30 kipindi kijacho cha majira ya joto kama mchezaji huru, baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya mshahara mpya anaoutaka wa pauni 400,000 kwa wiki. ***(Mirror)***

### JONES AWANIWA LEEDS
MLINZI wa Manchester United, Phil Jones mwenye umri wa miaka 30 yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaowaniwa na Leeds United, lakini Southampton na Fulham zinamtaka. ***(Marca)***

### ZINCHENKO KUACHIWA CITY
MANCHESTER City ipo tayari kumwachia, Oleksandr Zinchenko mwenye umri wa miaka 25, huku Everton ikiripotiwa kumwania nyota huyo wa kimataifa wa Ukraine. ***(Fabrizio Romano)***

### WILLIAMS KUONDOKA LIVER
LIVERPOOL imemwambia mlinzi, Neco Williams mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuondoka kwa mkopo, huku Nottingham Forest ikimtaka nyota huyo wa kimataifa wa Wales. ***(Mirror)***

### ARSENAL YANYIMWA MARTINEZ
KLABU ya Ajax imekataa ofa ya pauni milioni 25 kutoka Arsenal kwa ajili ya kumuuza nyota wao wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 24, Lisandro Martinez. ***(Mail)***

### CISSE AMULIKWA ENGLAND
KLABU za Brighton na Watford zinamwania mlinzi wa Olympiakos mwenye umri wa miaka, 26 Pape Abou Cisse raia wa Senegal. ***(Star)***

### FERGUSON AWINDWA MILWALL
KLABU ya Millwall imetoa ofa kwa Aberdeen ya pauni milioni 1.5 kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kimataifa wa Scotland, Lewis Ferguson mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR ATAKA KUMALIZA MKATABA WAKE NA PSG

●●●Ni kweli kwa upande wangu nataka kubaki, hakuna aliyeniambia chochote, lakini kwa…

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR hana nia ya kuondoka Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto licha ya tetesi kudai kwamba, nyota huyo wa Brazil yupo kwenye mipango ya kuachana na klabu hiyo.

Ripoti kutoka Ufaransa zimeeleza kuwa PSG wako tayari kuachana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, katika jitihada za kupunguza bili yao ya mishahara inayozidi kupanda.

Hiyo ni baada ya Kylian Mbappe kuongeza mkataba mpya unaomfanya kulipwa mshahara mkubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote ndani ya klabu hiyo.

Mabingwa hao wa Ligue 1 wamekuwa na kazi kubwa ya kuongeza kikosi chao katika soko la uhamisho wa majira haya ya joto.

Hivi sasa wanapambana wakimtaka Nuno Mendes kutoka Sporting CP kwa mkataba wa kudumu, huku pia wamekifikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa Porto, Vitinha kwa euro milioni 40.

Neymar bado ana miaka mitatu kwenye mkataba wake aliosaini mwaka 2021, na hivi majuzi aliliambia Jarida la Oh My Goal kuhusu mipango yake ya baadaye: "Ni kweli kwa upande wangu kwamba, nataka kubaki.

"Hakuna mtu aliyeniambia chochote, lakini kwa upande wangu, ni wazi nataka kubaki.

Hilo liko wazi kwa sababu nina miaka mitatu kwenye mkataba wangu wa sasa, sina sababu yoyote ya kuondoka, ingawa sijazungumza lolote na viongozi wa PSG.

Pamoja na kutoa kauli hiyo, Neymar ameendelea kuhusishwa na kutaka kuondoka, licha ya kwamba klabu nyingi zitapata wakati mgumu kufikia mshahara wake mkubwa.

Jarida la Hispania la Marca lilimkariri akisema kwamba, hana nia ya kuondoka, na kwamba anataka kumaliza muda wake hapo PSG.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 260,
MECHI KALI
NAMUNGO
VERSUS
COASTAL UNION
1 | 2.19
X | 2.75
2 | 3.58
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# NKETIAH AJIFUNGA MIAKA MITANO MINGINE ARSENAL

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Eddie Nketiah amekubali kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na 'Washikabunduki' hao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye mkataba wake ulikuwa unamalizika mwishoni mwa mwezi huu, amecheza mechi 92 kwenye kikosi cha kwanza na kufunga mabao 23 tangu aanze kikosi cha kwanza mwaka 2017.

Alimaliza msimu uliopita akiwa katika kiwango kizuri, akianza mechi nane zilizopita za ligi za Arsenal na kufunga mabao matano.

"Nimefurahi Eddie kubaki nasi," alisema kocha Mikel Arteta.

"Anawakilisha kile tunachohusu na maadili yote ya klabu.

"Tuna furaha sana kwamba, ameongeza mkataba wake na sasa lazima tufanye kazi na kuendelea kukuza kipaji chake kikubwa na mtu ambaye tunaye ndani yake."

Mchezaji huyo wa London, ambaye atavaa jezi namba 14 msimu ujao, akiwa amevaa nambari 30 hapo awali, alicheza mechi yake ya kwanza nyumbani kwa mabao mawili dhidi ya Norwich City kwenye Kombe la Carabao mwaka 2017 na kushiriki michuano ya Kombe la FA na alikuwa kwenye kikosi kilichokuwa kikishinda Ngao ya Jamii mwaka 2020.

Pia ndiye mfungaji bora wa muda wote wa timu ya Taifa ya England ya Vijana chini ya umri wa miaka 21 akiwa amefunga mabao 16 katika mechi 17 alizocheza na kuwa nahodha wa kikosi kilichoshinda mashindano ya Ulaya ya umri huo msimu wa 2021/2021.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Arsenal, Edu, aliongeza: "Misingi ya kikosi hiki imejengwa kwenye vipaji vya vijana na hasa wale waliokuja kupitia mfumo wetu wa akademi."

# Dembele: Nataka kubaki Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

OUSMANE Dembele ana nia ya kubaki Barcelona na amekanusha vikali uvumi unaomhusisha na kujiunga na Chelsea na kusema "uvumi tu" - katika mahojiano ya papo kwa hapo barabarani wakati akisubiri kuruhusiwa na taa za kuongozea magari.

Barcelona ililipa kitita cha euro milioni 105 kumnunua Dembele kutoka Borussia Dortmund mwaka 2017, lakini mkataba wa miaka mitano aliosaini unatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwezi huu.

Bayern Munich na Chelsea zinaripotiwa kumtaka mshindi huyo wa Kombe la Dunia, ambaye aliambiwa hadharani kuondoka Barca na klabu hiyo wakati wa dirisha la usajili la Januari baada ya mazungumzo ya mkataba mpya kuvunjika.

Hata hivyo, bila harakati yoyote iliyofanyika kabla ya mwisho wa Januari, Dembele alijumuishwa kwenye kikosi cha Xavi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alimaliza msimu akiwa na pasi nyingi za mabao, 13 kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye LaLiga.

Rais wa Barcelona, Joan Laporta amesisitiza nia yake ya kutaka kumbakisha Dembele katika klabu hiyo, na mkuu huyo wa 'Blaugrana' anaonekana kutekeleza matakwa yake.

Akiwa amekwama kwenye foleni ya magari barabarani, Dembele aliulizwa maswali na shabiki kwenye gari la pembeni yake, na mahojiano hayo yakatumwa kwenye mitandao ya kijamii.

Alipoulizwa kama angebaki katika klabu hiyo, winga huyo alijibu tu



"ndiyo".

Alipobanwa kuhusu kutakiwa Chelsea, Dembele alisema; "huo ni uvumi tu" na kuongeza "najisikia furaha sana nikiwa Barcelona".

Maoni hayo kutoka kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa yatakuwa chachu kwa Barcelona huku Xavi akitarajia kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu mpya wa 2022-23.

,838,830

# MGUNDA: HAKUNA CHA AJABU AKPAN KUJIUNGA NA SIMBA SC

**Na Cheji Bakari, Tanga**

BAADA ya taarifa kuenea kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari kuwa kiungo tegemeo wa Coastal Union, Mnigeria Victor Akpan, tayari amesajiliwa na Klabu ya Simba kuelekea msimu mpya wa 2022/23, Kocha Mkuu wa 'Wagosi wa Kaya' hao, Juma Mgunda (pichani), alisema hakuna geni katika suala hilo kwa kuwa ni jambo la kawaida.

Simba ipo katika mkakati mzito wa kuimarisha kikosi chao kuelekea msimu ujao kutokana na msimu huu kupoteza mataji yake matatu dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga; ambayo ilianza msimu kwa kuipokonya Ngao ya Jamii, kisha ikainyang'anya ubingwa wa Ligi Kuu Bara na sasa inaelekea fainali ya Kombe la FA baada ya kuwatupa nje mahasimu wao hao.



Akizungumza na mwandishi wa habari hizi kwa njia ya simu kutoka mjini Lindi ambapo Coastal Union leo, Jumatatu inacheza na Namungo FC kwenye mechi ya Ligi Kuu, alisema yeye pia anazisikia habari hizo za Akpan kumalizana na Simba, lakini hayo ni mambo ya kawaida kwenye timu na ana haki ya kufanya hivyo.

"Hizo habari zipo na ni za kawaida kwenye timu kwa kipindi hiki, kama inatokea hivyo basi ni haki yake, lakini Akpan huku tunaye kwa ajili ya maandalizi ya kucheza na Namungo FC kesho (leo)," alisema. Akpan ambaye amekuwa ni moja ya wachezaji wenye msaada mkubwa ndani ya kikosi cha Wagosi wa Kaya ambapo kwenye mechi iliyopita dhidi ya Yanga licha ya kufungwa mabao 3-0 yeye pamoja na Abdul Hamisi Selemani " Sopu" walikuwa kivutio kwa kuichezesha timu vizuri.

Mwishoni mwa wiki iliyopita taarifa zilienea kupitia vyombo mbalimbali vya habari kuwa kiungo huyo amesaini mkataba wa kuitumikia Simba msimu ujao wa Ligi Kuu Bara na mashindano mengine.

Taarifa hizo zilizidi kufafanua kuwa Coastal Union imeridhia kumwachia kiungo huyo kwenda Simba kwa dau la shilingi milioni 100.

# Yanga kuweka kambi Uturuki

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imetangaza rasmi kuwa itaweka kambi ya wiki tatu nje ya nchi kujiandaa na msimu ujao wa mashindano yote ya ndani ya nje ya nchi.

Makamu Mwenyekiti wa Mashindano wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said (pichani), amesema kuwa baada ya kumaliza fainali ya Kombe la FA Julai 12, watawapa wachezaji mapumziko kwa siku 10 tu, kabla ya kukusanyika tena kwa ajili ya msimu mpya wa ligi, kwani Ligi ya Mabingwa Afrika itaanza kati ya Agosti 12 na 14. Hata hivyo, hakutaka kuitaja nchi ambayo timu hiyo itakwenda kupiga kambi 'Preseason', lakini taarifa ambazo zimelifika gazeti hili kutoka chanzo chetu ndani ya klabu hiyo zinaeleza kwamba hadi sasa nchi ambayo wanaweza kwenda ni Uturuki.



"Tunamaliza ligi tarehe 29, Julai 2 tutacheza fainali ya Kombe la FA, ukiangalia hapo muda ni mchache, tutawapa mapumziko ya siku 10 tu wachezaji wetu tutataka hadi Julai 15 wawe wameripoti kwa ajili ya kujiandaa na mazoezi ya mwanzo wa msimu, tutakwenda nje ya nchi kujiandaa kwa wiki tatu, na baada ya hapo tutarejea nchini kwa ajili ya maandalizi ya Siku ya Mwananchi Agosti 6, mwaka huu.

"Baada ya hapo wiki moja tu inayofuata tutaanza mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa, hatujui, huenda tukaianza nyumbani au ugenini, hapo unaweza kuona kabisa kuwa muda ni mchache, lakini hiyo ndiyo ratiba yetu ya kuanzia msimu ujao wa mashindano," alisema Hersi.

Kuhusu usajili, Hersi ambaye tayari amechukua fomu kugombea urais wa klabu hiyo, amesema mpaka sasa wamesajili wachezaji wanne wa kigeni, na mmoja tayari wameshamtangaza, hivyo wamebaki watatu ambao wataanza kuwaweka hadharani hivi karibuni.


JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 .21/06/22 | 22:30 | Levadia Tallinn vs Vikingur Reykjavik | 2.65 | 3.35 | 2.47 |
| 02 .22/06/22 | 01:00 | Aldosivi vs CA Platense | 2.74 | 2.99 | 2.50 |
| 03 .22/06/22 | 03:30 | Central Cordoba vs San Lorenzo | 2.33 | 3.00 | 2.95 |
| 04 .22/06/22 | 13:00 | Gamba Osaka vs Oita Trinita | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 05 .22/06/22 | 13:30 | Bucheon vs Anyang | 2.41 | 3.10 | 2.76 |
| 06 .22/06/22 | 18:00 | Seinajoen JK vs Haka | 2.44 | 3.05 | 2.76 |
| 07 .22/06/22 | 18:30 | Japs vs MP Mikkeli | 2.24 | 3.30 | 2.86 |
| 08 .23/06/22 | 00:00 | Resistencia FC vs 12 de Octubre de Itaugua | 2.38 | 2.99 | 2.89 |
| 09 .23/06/22 | 01:30 | Bahia BA vs Atletico Pr | 2.62 | 2.91 | 2.67 |
| 10 .23/06/22 | 02:00 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.31 | 3.00 | 3.00 |
| 11 .23/06/22 | 03:00 | NY Red Bulls vs New York City | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 12 .24/06/22 | 02:00 | Sao Paulo vs Palmeiras | 2.70 | 3.04 | 2.50 |
| 13 .24/06/22 | 03:30 | CSA AL vs Gremio | 3.15 | 2.85 | 2.32 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 20/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1305 | Sheikh Russel KC vs Sheikh Jamal | 4.22 | 3.44 | 1.75 |
| 13:00 | 3142 | Sebeta City FC vs Hadiya Hosahina FC | 3.44 | 2.85 | 2.18 |
| 13:00 | 3314 | Rahmatgonj Mfs vs Bashundhara Kings | 10.76 | 5.68 | 1.20 |
| 13:00 | 3458 | Mohammedan Sporting Club Dhaka vs Dhaka Abahani | 4.93 | 3.55 | 1.63 |
| 14:30 | 1342 | Shanghai Shenhua vs Wuhan Zall | 2.14 | 3.14 | 3.19 |
| 14:30 | 4019 | Anhui Litian vs Sichuan Jiuniu | 2.07 | 3.35 | 3.15 |
| 14:30 | 5605 | Guangzhou RF vs Hangzhou NG | 5.48 | 3.81 | 1.53 |
| 15:00 | 4106 | San Lorenzo de Almagro Res. vs CA Central Cordoba SE Reserve | 2.40 | 3.10 | 2.95 |
| 15:00 | 4957 | Racing Club Reserve vs Gimnasia de la Plata Reserve | 2.60 | 3.30 | 2.55 |
| 16:00 | 2496 | Ethiopia Bunna SC vs Addis Ababa City FC | 2.33 | 2.76 | 3.25 |
| 16:00 | 3401 | Namungo vs Coastal Union | 2.19 | 2.75 | 3.58 |
| 17:00 | 4010 | Argentinos Juniors Reserve vs Newells Old Boys | 1.75 | 3.48 | 4.12 |
| 17:00 | 4180 | FC Norchi Dinamo Tbilisi vs WIT Georgia | 2.21 | 3.24 | 2.95 |
| 17:00 | 4277 | CA Platense vs CA Aldosivi Reserve | 2.41 | 3.18 | 2.69 |
| 17:00 | 5470 | Defensa Y Justicia Reserve vs CD Godoy Cruz | 1.68 | 3.75 | 4.60 |
| 18:00 | 2319 | Egersund IK vs Odds BK 2 | 1.54 | 4.52 | 4.33 |
| 18:00 | 4248 | Start 2 vs Sarpsborg Sparta 2 | 2.28 | 3.69 | 2.56 |
| 18:30 | 2811 | Innstrandens IL vs Rosenborg BK 2 | 4.71 | 4.91 | 1.46 |
| 19:00 | 1222 | Kongsvinger IL vs Grorud IL | 1.82 | 3.74 | 3.54 |
| 19:00 | 2897 | Sandnes Ulf vs Kfum Oslo | 2.43 | 3.29 | 2.60 |
| 19:00 | 3001 | Baerum vs Valerenga IF 2 | 1.48 | 4.61 | 4.81 |
| 19:00 | 4770 | Aasane Fotball vs Ranheim | 2.86 | 3.45 | 2.18 |
| 19:00 | 4838 | FC Elva vs Viljandi Tulevik | 1.30 | 5.66 | 7.89 |
| 19:00 | 5566 | Skeid Fotball vs Sogndal | 2.80 | 3.34 | 2.26 |
| 19:30 | 2362 | FK Haugesund 2 vs Stord | 2.99 | 4.12 | 1.91 |
| 20:00 | 1875 | Nordstrand vs Kjelsaas 2 | 1.31 | 5.27 | 6.84 |
| 20:00 | 3081 | Grei vs Stabaek Fotball 2 | 3.58 | 4.02 | 1.75 |
| 20:00 | 3365 | Hammarby Talang FF vs Taby FK | 2.00 | 3.68 | 3.04 |
| 21:00 | 3171 | EC Prospera SC vs Azuniz FC | 5.12 | 3.05 | 1.73 |
| 21:00 | 3293 | Fram Reykjavik vs Vestmannaeyjar | 1.98 | 3.54 | 3.19 |
| 21:00 | 5984 | CA Atlanta vs Mitre SdE | 1.93 | 3.34 | 3.54 |
| 21:30 | 5201 | Sportivo Italiano vs Excursionistas | 2.35 | 2.84 | 3.09 |
| 21:30 | 5402 | Talleres RDE vs Justo Jose De Urquiza | 2.05 | 2.80 | 3.93 |
| 21:30 | 5687 | Brown Adrogue vs Defensores Belgrano | 2.22 | 2.94 | 3.23 |
| 22:00 | 3971 | CA Boston River vs Danubio FC | 2.19 | 2.99 | 3.24 |
| 22:15 | 4150 | Breidablik vs KA Akureyri | 1.66 | 3.83 | 4.22 |
| 22:15 | 5522 | Stjarnan vs KR Reykjavik | 2.74 | 3.53 | 2.21 |
| 22:30 | 5974 | Godoy Cruz vs Defensa Justicia | 2.34 | 3.15 | 2.81 |
| 23:00 | 4290 | Ayacucho vs Sport Huancayo | 2.95 | 3.25 | 2.20 |


JUMANNE - 21/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4779 | Daejeon Citizen vs Gwangju | 2.69 | 3.14 | 2.44 |
| 13:30 | 3881 | Gimpo Citizen vs Jeonnam Dragons | 2.60 | 3.09 | 2.55 |
| 13:30 | 5223 | Suwon City vs Pohang Steelers | 3.14 | 3.29 | 2.09 |
| 13:30 | 5381 | Daegu vs Jeju Utd | 2.70 | 3.04 | 2.50 |
| 14:30 | 1462 | Shandong Luneng vs Dalian Aerbing | 1.33 | 4.53 | 7.88 |
| 16:00 | 5318 | La Fiorita vs Inter Club De Escaldes | 5.40 | 3.55 | 1.63 |
| 18:30 | 1048 | Slovakia U19 vs Italy U19 | 6.85 | 4.80 | 1.34 |
| 18:30 | 4714 | FC Vaajakoski vs Vifk Vaasa | 2.07 | 3.59 | 2.95 |
| 20:00 | 3796 | Zenit St Petersburg vs Nizhny Novgorod | 1.35 | 4.62 | 7.08 |
| 22:30 | 1469 | Levadia Tallinn vs Vikingur Reykjavik | 2.65 | 3.35 | 2.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Juni 20, 2022
Nipashe



**Neymar ataka kumaliza mkataba wake na PSG**

TUNATISHA...



Mashabiki wa Simba wakishangilia moja ya mechi za Ligi ya Mabingwa za timu yao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTBA**

# SIMBA YAONYESHA UKUBWA WAKE CAF

● ● ● Sasa kuanzia raundi ya kwanza Ligi ya Mabingwa wakati Yanga ikianzia raundi ya awali baada ya...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), likitangaza msimu wake wa michuano Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika utaanza rasmi Agosti 12, mwaka huu, wawakilishi wa Tanzania wenye historia nzuri katika mashindano hayo, Klabu ya Simba itakuwa miongoni mwa klabu 10-bora zitakazoanzia raundi ya kwanza.

Kwa upande wa Tanzania, tayari wawakilishi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wamejulikana, ambao ni mabingwa wapya wa Ligi Kuu Bara, Yanga pamoja na Simba iliyojihakikishia kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ikumbukwe msimu ujao wa michuano ya CAF, Tanzania itawakilishwa na timu nne, mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, ambapo hadi sasa mchuano ni mkali kwenye Ligi Kuu timu zikiwania kumaliza nafasi nne za juu.

Hata hivyo, kama Yanga iliyotinga Fainali ya Kombe la FA, itafanikiwa kutwaa taji hilo dhidi ya Coastal Union, hiyo inamaana timu zitakazoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ndizo zitakazoiwakilisha nchi Kombe la Shirikisho Afrika, lakini Coastal ikilitwaa, itaungana na mshindi wa tatu wa Ligi Kuu kushiriki kinyang'anyiro hicho cha kimataifa.

Kwa mujibu wa Kanuni za CAF, klabu zinazoshika nafasi 10-bora kwenye viwango vya Shirikisho hilo, kama zitafuzu kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa kulingana na kanuni za mashirikisho ya nchi zao, ndizo ambazo huanzia raundi ya kwanza (First Round) na ambazo zipo nje ya 10-bora huanzia raundi ya awali (Preliminary Round).

Hata hivyo, Simba licha ya kushika nafasi ya 14-bora kwenye viwango vya klabu vya CAF, imeangukia kuanzia raundi ya kwanza baada ya Klabu ya RS Berkane iliyokuwa nafasi ya tano kwa ubora, Pyramids (9), Étoile du Sahel (10) na Orlando Pirates (11), kushindwa kufuzu michuano hiyo kupitia ligi za nchi zao.

Katika viwango vya Klabu vya CAF vilivyotolewa wiki iliyopita, namba moja inashikiliwa na Al Ahly ikifuatiwa na Wydad Casablanca, Espérance de Tunis, Raja Casablanca, RS Berkane, Mamelodi Sundowns, TP Mazembe, Zamalek, Pyramids, Étoile du Sahel, Orlando Pirates, Horoya FC, Petro de Luanda na Simba ikishika nafasi ya 14.

Kwa maana hiyo, kushindwa kufuzu michuano hiyo kwa Klabu za RS Berkane, Pyramids, Étoile du Sahel na Orlando Pirates, moja kwa moja zinatoa nafasi kwa Horoya FC iliyokuwa nafasi ya 12, Petro de Luanda (13) na Simba nafasi ya 14, kupanda na kuingia ndani ya klabu kumi bora zitakazoanzia michuano hiyo raundi ya kwanza.

Hivyo, Simba, Horoya FC na Petro de Luanda zitaungana na Al Ahly, Wydad Casablanca, Espérance de Tunis, Raja Casablanca, Mamelodi Sundowns, TP Mazembe pamoja na Zamalek kuwa klabu 10 zitakazoanzia raundi ya kwanza kwenye michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri barani Afrika kwa ngazi ya klabu.

Nafasi ya Simba kuingia hatua hiyo imetokana hasa na Étoile du Sahel kupoteza mchezo wao wa mwisho dhidi ya Monastir kwa kuchapwa mabao 2-0 ugenini juzi, hivyo kukosa nafasi ya kuongoza kundi lao kwenye Ligi Kuu Tunisia, na kutoa nafasi kwa Club Africain kuongoza kundi na kufuzu Ligi ya Mabingwa, ambapo sasa itakuwa miongoni mwa zikazoanzia raundi ya awali.

Wawakilishi wengine wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa, Yanga ambao wametwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu, pamoja na klabu zingine zilizofuzu Ligi ya Mabingwa ambazo hazipo kwenye 10-bora, wao wataanzia raundi ya awali na kama wakipata matokeo ya jumla nyumbani na ugenini, wataingia kwenye droo ya kupangiwa moja kati ya klabu 10-bora hizo, kucheza tena mechi ya nyumbani na ugenini ili kusaka nafasi ya kufuzu hatua ya makundi.

## Mayele, Mpole wategana Kiatu

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

VINARA wa kucheka na nyavu Ligi Kuu Bara, Fiston Mayele wa Yanga na George Mpole wa Geita Gold FC, ni kama wameanza kuwekeana mitego kwa kila mmoja kuzuga kama hawazii kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa kuibuka mfungaji bora wa ligi hiyo mwishoni mwa msimu.

Mayele na Mpole kila mmoja ana mabao 16 wakati huu Yanga ikiwa imebakiza mechi tatu na Geita Gold michezo miwili kabla ya msimu wa Ligi Kuu 2021/22 kumalizika hapo Juni 29, mwaka huu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti na waandishi wetu, kila mmoja ameweka wazi kuwa lengo lake ni kuipa timu matokeo na si kuwazia kumaliza kinara wa ufungaji katika ligi hiyo.

Mayele alimwambia mwandishi wetu juzi kuwa kwa upande wake anahitaji kutafuta matokeo kwa ajili ya kusaidia timu yake na hataki presha ya kuwaza anashindanishwa na nani katika mbio za kuwania tuzo ya ufungaji bora.

"Tulitaka ubingwa, hilo tumefanikiwa na sasa hivi hakuna tunachokitafuta ni kumaliza ligi bila kufungwa nahitaji kusaidia timu yangu kupata matokeo na si ushindani na Mpole kuwa mfungaji bora," alisema Mayele.

Wakati Mayele akieleza hayo, Mpole alisema lengo ni kufunga magoli katika michezo yao iliyobakia ili washike nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Lengo ni kushika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hii japokuwa ina ushindani mkubwa," alisema Mpole.

Mpole alisema anawashukuru mashabiki kwa ushirikiano wanaoendelea kuwaonyesha katika kipindi hiki cha Ligi Kuu ya NBC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >